# Nipashe

Jumatano Agosti 3, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581026 *

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11


BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT

1,019,301,493/-

KWA 1000/- TU!

SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#




## CCM yazimulika nyayo wapanga safu na wasaliti

UKURASA 3



# Kishindo cha bomoabomoa

• **Waziri** asisitiza kitaendelea kwa sababu... *Endelea Uk.2*



Rais Samia Suluhu Hassan akimpatia maelezo kuhusu picha mgeni wake, Rais wa Jamhuri ya Zambia, Hakainde Hichilema na baadaye kumkabidhi zawadi hiyo Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Mshtakiwa alikana begi lenye meno ya tembo

UKURASA 3

# Samia, Rais wa Zambia kusaka fedha ujenzi SGR

UKURASA 2


**MICHEZO** **SIMBA YAANZA VITISHO YANGA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Kishindo cha bomoabomoa

Na Romana Mallya

SERIKALI imesema bomoabomoa inayoshuhudiwa sasa mkoani Dar es Salaam inatokana na wamiliki wa maeneo yaliyovamiwa, kushinda kesi mahakamani.

Akizungumza na Nipashe jana kuhusu bomoabomoa iliyoshuhudiwa wiki iliyopita katika maeneo ya Mabwepande na Kimbesa Mpijimagohe, Manispaa ya Ubungo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, alisema ubomoaji unatekelezwa chini ya utawala wa mkoa husika.

"Kwa sababu ni uvunjaji wa sheria kwa maana ya uvamizi wa maeneo, Mkuu wa Mkoa ndiye anaweza kujua zaidi. "Ninaomba msaidie kuelimisha kwa sababu Dar es Salaam ndiyo wengi wamepigwa. Wananchi wasinunue viwanja kwa mtu na kuridhika, anunue kiwanja kwa kujiridhisha halmashauri kama aliyemuulizia ni mmiliki kweli, hiyo tu ndiyo itakayowasaidia," alisema.

Alipoulizwa kama bomoabomoa hiyo ni kwa Mkoa wa Dar es Salaam pekee, Waziri Mabula alisema itaigusa pia mikoa mingine kwa kutegemea na kuwapo uvamizi.

"Mtu anapokwenda kushtaki kudai haki yake na hao wengi wao wameshinda mahakamani, siwezi kujua ni mkoa upi na upi mikoa ndiyo inayojua," alifafanua.

Alisema kesi zinapotoka mahakamani baada ya ushindi, anayetekeleza hukumu ni mtawala wa eneo ama mkuu wa wilaya, ofisa tarafa au mkuu wa mkoa.

"Sisi siyo watekelezaji hukumu za mahakama, tunatekeleza sheria kwa maana ya kusema nani ni nani kwenye umiliki. Wanapokwenda mahakamani, ofisa wa ardhi anaitwa ili kusema kama hati ni za ukweli.

"Waliobomolewa wengi ni waathirika ambao waliuziwa na huwa tunawaambia ukitaka kupata eneo usiende kwa mtu tu, mtu sawa utapatana naye lakini nendeni halmashauri mjiridhishe kiwanja ni cha kwake? Hii itawafanya watu wasipate athari," alisema.

Waziri Mabula alitoa wito kwa mwananchi yeyote anayehitaji kiwanja, hasa maeneo ya majiji, manispaa na miji, asinunue kwa kufuata ushahidi wa mwenyekiti tu.

Alisema anatakiwa aende halmashauri kujiridhisha, kiwanja anachotaka kununua kama anayemuuzia ni mmiliki halali na kama kimepimwa. "Msinunue kwa kupeana tu, hata hawa wengi wanalalamika kwamba mwenyekiti alinipa barua. Mwenyekiti hana mamlaka ya kugawa kwenye maeneo ambayo yana thamani kubwa.

"Taratibu za mipango miji, mwenyekiti hana nafasi, mwenyekiti ana nafasi kwenye halmashauri za wilaya huko vijijini. Sheria Na. 5 na yeye pia hana mamlaka kama yeye, lazima apeleke kwenye mkutano wa mkuu wa kijiji, ndipo waidhinishe mtu kupewa ardhi. Hata kama anapewa kipande, lazima wamtambue. "Hawa waliopo mijini wanaonunua kupitia kwa wenyeviti au kuuziwa na watu wengine wanavamia maeneo halafu akivamia anatafuta mnunuzi anajitoa, kesi inakuwa siyo yake ndipo migogoro inapoanza," alisema.

Alihoji maeneo ambayo yapo chini ya mipango miji mtu anakwendaje kuuziwa na mwenyekiti ambaye hana mamlaka hiyo?, akisisitiza yapo chini ya Sheria Na. 8 na 4 za Ardhi.

Waziri huyo alisema anasikitika kuona wananchi wengi wamepoteza nguvu zao kujenga halafu nyumba zinaangushwa.

Kuhusu bomoabomoa hiyo kuhusisha baadhi ya nyumba na nyingine kuachwa, waziri huyo alisema yapo maeneo ambayo mwenye ardhi alitaka kupewa fidia kwa kukubaliana kama mtu anataka kubaki, alipe ardhi hiyo.

"Sina uhakika kama hao walioachwa walilipa ardhi au kuna maeneo mengine ambako huenda kuna makosa yamefanyika watu wamepewa hati.

"Sasa akipewa hati lazima washtakiane, huwezi kumvunjia kwa sababu serikali ilimpa hati na kama amepewa hati ndani ya kiwanja cha mtu, hapo inabidi wizara iingie kujua nani ni mmiliki halali, ila kwa vyovyote aliyeanza kupewa hati ndiyo mwenye ardhi," alifafanua.

Alisema inapotokea hivyo, huyo mwingine wizara inaweza kuingia hasara kwa maana inamtafutia kiwanja sehemu nyingine kwa sababu makosa hapo huwa ni ya wizara.

"Hili hufanywa na wizara mara nyingi pale kunapotokea kunakuwa na kesi za aina hiyo, lakini hao wengine unaowaona wameachwa siwezi kujua, pengine wamekubaliana na mwenye eneo atalipa ardhi au namna gani, hapo kesi inashughulikiwa na mkuu wa mkoa," alifafanua.

Kuhusu kauli iliyotolewa awali ya mapori ambayo hayajaendelezwa wapewe wananchi, waziri huyo alisema mtu hawezi kuingia kwa amri hiyo tu.

"Yaani mwananchi kuingia ni mpaka pale ardhi husika iwe imebatilishwa na hapo sasa tumepeleka mashamba mengi ambayo ni mapori kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ili kuyabatilisha, nimeshawaagiza makamishna kila mkoa wapite viwanja vyote ambavyo vimeachwa na vimeshakuwa mapori na kuleta hali ya hatari, waanze kutumia taratibu za kisheria kuanza kuwang'anya na kwenye hili lazima watoe notisi.

"Hili linafanywa kwa kufuata sheria, huwezi tu ukavamia. Ukivamia, unakuwa bado ni mvamizi, mhusika bado atakuwa na hati, atakuwa bado hajanyang'anywa na kubatilisha," alisema.

**WALIOKUMBWA NA BAA**

Mjumbe wa Shina Na. 6 Tawi la Kinondoni, Mtaa wa Mji Mpya, Kata ya Mabwepande wilayani Kinondoni, Abdallah Gombero, akizungumza na Nipashe, alidai ubomoaji kwenye eneo lao hilo ulifanyika Juni 16 mwaka huu pasina wananchi kupewa taarifa au amri ya mahakama, zaidi ya nyumba 300 zikikumbwa na baa hilo.

"Nyumba yangu kama mjumbe imebomolewa, ina thamani ya Sh. milioni 16. Huku niliingia mwaka 2013, haya yalikuwa mashamba pori, serikali ya kijiji ndiyo ilikuwa inatugawia na amri ilitoka kwa Mkuu wa Mkoa wa kipindi hicho, Rita Mlaki," alidai.

Amina Rashid, mwathirika mwingine wa bomoabomoa hiyo kwenye eneo la Mji Mpya, alisema: "Juni 16, 2022 wakati wanafanya oparesheni hii ya kubomoa, nilikuwa wilayani (ofisi za wilaya), jokofu lipo humo ndani na vitu vyangu, ninapigiwa simu na mjumbe nyumba yako inashushwa. Nikauliza viongozi, mbunge na diwani wako wapi, akakata simu," alisema.

Mwathirika mwingine wa bomoabomoa hiyo, Abdallah Rashid, alidai walikumbana na baa hilo mwaka 2001 na walikimbilia mahakamani alikodai walishinda kesi, laki mwaka huu nyumba yake yenye thamani ya Sh. milioni 35 imebomolewa.

Utatuzi wa migogoro ya ardhi ni miongoni mwa vipaumbele vya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika mwaka huu wa fedha ambao sasa umeingia mwezi wa pili wa utekelezaji wake.

# Samia na Rais Zambia kusaka fedha ujenzi SGR

Na Romana Mallya

RAIS Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zambia, Hakainde Hichilema, wamekubaliana kushirikiana maeneo makubwa saba kwa ajili ya kuboresha uchumi, ikiwamo kuijenga upya reli ya TAZARA kuwa ya kisasa (SGR).

Makubaliano hayo yalifikiwa jana Ikulu jijini Dar es Salaam katika mazungumzo ya viongozi hao wakati wa ziara ya siku moja ya Rais Hichilema, ambapo pia kulishuhudiwa utiaji saini makubaliano eneo la usalama na utamaduni uliofanywa na mawaziri wa mambo ya nje wa nchi hizo.

Mbali na ushirikiano katika eneo la uchumi, maeneo mengine waliyokubaliana ni uhusiano wa kisiasa, usalama wa nchi hizo, uwekezaji, kutatua vikwazo vya madereva mipakani, kilimo na tume inayozungumzia nchi hizo mbili kukutana mara moja.

Akizungumza katika hafla hiyo, Rais Samia alisema katika mazungumzo yao, waligusia namna nchi hizo zilivyo karibu, zenye urafiki na undugu.

"Wazee wetu Julius Nyerere (Baba wa Taifa) na Kenneth Kaunda (Baba wa Taifa la Zambia) walituwekea misingi mizuri ya ushirikiano, lakini wazee hawa ndiyo walioshirikiana kuleta ukombozi kusini mwa Bara la Afrika, wakatuanzishia mambo ambayo walitaka yadumu milele na kutuunganisha.

"Tuliachiwa mabadiliko mbalimbali ya kiuchumi na siasa na yametufanya kidogo tutengeneze umbali baina yetu. Kwa maana hiyo, tumekubaliana na mwenzangu turudi kwenye udugu kama tulivyoachwa na wazazi wetu kwa kuangalia maeneo yote ambayo yatatufanya turudi," alisema.

Rais Samia alitaja jambo la kwanza kuwa wameangalia uhusiano wa kisiasa kwa nchi hizo na kwa yote yaliyotokea, lazima wahakikishe kwamba viongozi wa nchi wanaowaongoza wananchi waelewane vizuri.

"Pili, usalama wa nchi zetu. Tumeangalia kwenye ukanda huu mambo yanayotokea, ugaidi na mambo mengine kadhaa, tukasema turudi tuwe na ushirikiano mkubwa kwenye usalama wa nchi zetu," alisema.

Alilitaja jambo la tatu kuwa wameangalia hali ya uchumi na wameangalia miundombinu waliyoachiwa na waasisi wa mataifa hayo ambayo ni reli ya TAZARA na bomba la mafuta la TAZAMA.

"Leo TAZARA haihudumii vyema nchi zetu mbili, TAZAMA Pipeline lengo lake lililoanzishiwa na inavyofanya leo ni vitu viwili tofauti. Tumekubaliana tuiboreshe TAZARA kama tutaifanyia marekebisho reli iliyopo, tumekubaliana kwamba kwa dunia ya leo reli ni SGR.

"Tumekubaliana kuwa na mradi wa pamoja, tutafute fedha pamoja kupitia PPP (ushirikiano kati ya sekta binafsi na umma) na pengine na wenzetu marafiki waliotujengea hiyo reli tuone namna tutakavyoiboresha kwenye kiwango cha SGR," alisema.

Kwa upande wa TAZAMA, Rais Samia alisema madhumuni yake yalikuwa ni bomba lipeleke mafuta kwenye mtambo wa kusafisha na baadaye kuuzwa na kwamba malengo hayo yameshuka kwa kiasi kikubwa.

Pia alisema Zambia imebadilisha sera zake kwenye nishati na sasa wanakwenda kwenye kuagiza bidhaa ambazo zimetimia.

Rais Samia alisema wamekubaliana bomba hilo (TAZAMA) ni dogo, hivyo liwe kubwa litakalopeleka mafuta kwa wingi na Bandari ya Dar es Salaam na vituo vilivyopo visaidie kupunguza uhaba wa mafuta nchini mwao.

Mkuu wa Nchi alitaja eneo lingine ni uwekezaji ambapo kuna vikwazo vya kikodi na visivyo vya kikodi vinavyofanya biashara kati ya nchi isikue.

Alisema wamekubaliana sekta za uwekezaji na biashara, taasisi za kukusanya mapato na zinazoshughulika na ushuru, zikae ziangalie wapi wamekwama na nini kikwazo ili waviondoe.

Kuhusu tatizo la vurugu za madereva, Rais Samia alisema wamekubaliana kuziweka pamoja taasisi za madereva Tanzania na Zambia, ili kuzungumza na serikali na kuangalia matakwa yao kutatua matatizo na kuondoa vikwazo mipakani.

Alisema wameangalia sekta ya nishati, hasa mradi mkubwa wa umeme unaohusisha nchi tatu; Tanzania, Kenya na Zambia ujulikanao kama 'Grid Interconnectivity'.

Rais Samia alisema kila nchi imeanza kufanya shughuli zake na Tanzania inatarajia kuanza Januari mwakani kujenga njia kubwa ya usambazaji itakayounganisha Kenya na upande wa Zambia wameshaanza.

"Ni umeme unaotokana na maji, tukatambiana kidogo kasema yeye yupo karibu asilimia 80, nikasema na mimi hadi 2024 nitakuwa asilimia 80 na nikimaliza Rufuji na Rumakali nitakuwa asilimia 100," alisema.

Rais Samia alitaja eneo lingine walilozungumza ni kilimo ambapo Tanzania na Zambia ni nchi ambazo ni wazalishaji wa soya na soko lao ni China na huko nyuma walikuwa wakichanganya pamoja kupeleka bidhaa sokoni.

Rais Samia alisema jambo lingine ni kuhusu tume inayozungumza mambo ya nchi hizo ambayo mara ya mwisho kukutana ilikuwa mwaka 2016 na wamekubaliana ikutane haraka ili waliyozungumza yafanyiwe kazi.

Pia alisema wamekubaliana kufanya kazi kwa pamoja na endapo mmoja akiwa na soko, basi amwambie mwingine na Tanzania imewaalika kwenye soko la mbuzi na kondoo lililolipata Saudi Arabia.

Rais wa Zambia, Hichilema, alisema uhusiano baina ya Tanzania na Zambia ni urithi ambao Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere na Baba wa Taifa la Zambia, Kaunda, walielewa umuhimu wake wa kuunganisha mataifa hayo.

Alisema wanatakiwa kufanya kazi kwa pamoja kwa sababu walikuwa pamoja katika harakati za kupigania uhuru na tangu wakati huo, watu wa nchi hizo wamekuwa kitu kimoja.

## Watatu wauawa kikatili, wamo waliochomwa moto

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WATU watatu wameuawa katika matukio mawili tofauti ikiwamo mzee wa miaka 60 kukatwa mapanga na wengine wawili kuchomwa moto kwa tuhuma za wizi wa ng'ombe.

Matukio hayo yalitokea Agosti mosi na Julai 31, mwaka huu kwa nyakati tofauti huku tukio la kwanza likitokea katika Kijiji cha Nyida, majira ya saa tatu usiku.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Nyida, Kidoto Maganga, alisema Kabula Ngasa (60), aliuawa kwa kukatwa na mapanga sehemu mbalimbali za mwili na watu wasiojulikana. Alisema Ngasa aliuawa akiwa kwenye kibanda chake cha kuuza bidhaa ndogo ndogo na watu hao walipofika waliagiza pipi na soda, kisha kutenda unyama huo.

"Wakati watu hawa walipotaka kutekeleza mauaji, walimtuma mjukuu wa bibi huyo akawaletee maji ya kunywa ndani, aliporudi wakampiga kwa ubapa wa panga akaanguka chini na kuzimia, ndipo wakatumia mwanya huo kumuua bibi yake," alisema Maganga.

Diwani wa Kata ya Nyida, Selemani Seregeti, alithibitisha kutokea kwa mauaji hayo na kwamba waliotenda tukio hilo hawajafahamika na chanzo hakijajulikana.

Katika tukio lingine Kijiji cha Mwamala wilayani Shinyanga, Simbili Izengo (33) na Kashinje Malulu (32), waliuawa kwa kuchomwa moto kwa madai ya kujihusisha na wizi wa ng'ombe.

Akizungumza na gazeti hili, Mtendaji wa Kata ya Mwamala, Suzana Kanyange, alisema tukio hilo lilitokea Agosti mosi, mwaka huu, saa 12:30 asubuhi, baada ya wananchi wenye hasira kuwazingira na kuwashambulia kwa kipigo kisha kuwachoma moto.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Leonard Nyandahu, alithibisha kutokea kwa matukio hayo huku polisi wakiendelea na uchunguzi kwa ajili ya kuwabaini waliohusika.

Aidha, aliwataka wananchi kuacha kujichukulia sheria mkononi bali wafuate taratibu za kisheria, huku wakiwaomba watoe taarifa kwa waliohusika na mauaji hayo.

# Mshtakiwa akana begi lenye meno ya tembo

**Na Grace Gurisha**

MSHTAKIWA Hussein Abdallah anayetuhumiwa kukutwa na vipande vinane vya meno ya tembo, amekataa begi lililobeba meno hayo kwa madai kwamba halina jina lake wala alama ya mpelelezi wa kesi hiyo.

Pia amedai meno hayo ni ya shahidi wa upande wa mashtaka, Wilfred Ollomy ambaye ni Ofisa Ugavi kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa kuwa alikabidhiwa kienyeji bila kufuatwa utaratibu.

Abdallah alidai hayo jana wakati Ollomy akitoa ushahidi dhidi yake mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Evodia Kyaruzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu huku akimtaka shahidi huyo amwogope Mungu kwa kutokusema uongo.

Mshtakiwa alitoa pingamizi hilo baada ya Ollomy kuiomba mahakama ipokee hati ya makabidhiano, begi pamoja na vipande hivyo kama vielelezo katika kesi kwa madai kwamba hakuwahi kukutwa na vitu hivyo.

Alidai kwamba begi hilo lililotolewa mbele ya mahakama halina chata yoyote inayoonyesha ni lake, hivyo linaweza kupelekwa begi la mtu yeyote na mashahidi wakadai ni la lake. Kwa msingi huo, mshtakiwa huyo alipinga kielekezo hicho kupokewa na mahakama.

Pia, aliiomba mahakama isipokee hati ya makabidhiano kwa madai kwamba wakati wanakabidhiana vipande hivyo na kutia saini hati hiyo, yeye hakuwapo.

"Ninapinga vipande hivi visipokewe kwa sababu kilo zinazotajwa kwenye vielelezo hivi kwenye hati ya mashtaka hakuna," alidai Abdallah.

Baada ya Abdallah kutoa mapingamizi hayo, Hakimu Kyaruzi alipokea vielelezo vyote na kumweleza mshtakiwa kwamba hoja zake siyo za kisheria na pia anavyovieleza vipo kwenye ushahidi, hivyo atakuja kamuuliza mhusika.

Abdallah anakabiliwa na mashtaka ya kukutwa na nyara za serikali ambazo ni vipande vinane vya meno ya tembo vyenye thamani ya Dola za Marekani 15,000, sawa na Sh. milioni 94.5.

Awali, Ollomy alidai Januari 4, 2019, majira saa tano usiku, alipigiwa simu na Ofisa Wanyamapori, Madimi Tumbo, akimtaka kufika Kituo cha Polisi Mburahati, Dar es Salaam kwa ajili ya kuchukua nyara zilizokamatwa na kuzihifadhi.

Alidai alipofika kituoni huko, alikabidhiwa vipande vinane vya meno ya tembo vilivyosajiliwa kwa namba MBS 1-8 na MBT/RB/99/2019.



Wanafunzi wanaosoma Shule ya Msingi Nyamalogo, wilayani Shinyanga, wakitoka shuleni kurejea nyumbani kwa kutumia usafiri wa tela linalokokotwa na ng'ombe, juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# CCM yamulika nyayo wapanga safu, wasaliti

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimesema kinafuatilia kwa karibu malalamiko na mienendo ya uchaguzi wake wa ndani huku kikitaka viongozi waroho wa madaraka, wala rushwa na wapenda sifa kutochaguliwa.

Kwa nyakati tofauti jana, Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo akiwa Hai mkoani Kilimanjaro na Katibu wa Halmashauri Kuu ya chama hicho (NEC) Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka akiwa jijini Dodoma, walisisitiza katiba na kanuni za uchaguzi kuzingatiwa.

Nipashe ilimuuliza Shaka kuhusu rafu zinazoendelea kwenye uchaguzi huo, akijibu: "Uchaguzi kwa ujumla tunafuatilia kwa karibu sana, malalamiko ya wanachama yanayotolewa kwenye ngazi mbalimbali, kwa asilimia 80 hadi 85 unakwenda vizuri.

"Bahati nzuri sana hivi sasa utandawazi umekua. Kwa hiyo, kama kanuni ya uchaguzi inaelekeza upeleke malalamiko kwenye ngazi husika, kutokana na kukua kwa utandawazi tumekuwa tukipokea hata ngazi ya makao makuu.

Jambo hili linatusaidia kufuatilia kwa karibu sana kwenye ngazi husika, niendelee kuwasihi wanachama ambao wameomba nafasi za uongozi na wanaona hawatendewi haki, nafasi wanayo kwa mujibu wa katiba na kanuni za uchaguzi ya kulalamika na kuwasilisha malalamiko ngazi za juu zinazohusika."

Alisisitiza kuwa vikwazo vya kikatiba na kikanuni vya moja kwa moja, chama kimeelekeza ngazi zinazohusika kuhakikisha zinasimama kwenye msingi mkuu wa chama.

"Katika kusimama kwenye msingi mkuu wahakikishe wanasimama kwenye haki. Ili kujenga imani kwa wanachama, lazima haki itendeke. Msisitizo wetu mkubwa ni kuishi kwenye katiba na kanuni tulizojiwekea katika kusimamia haki za wanachama wetu," alisema.

Shaka aliwataka wajumbe wa vikao vya kikanuni vya ngazi mbalimbali vinavyopokea malalamiko kuhakikisha kwamba wanasimamia misingi ya kutenda haki.

Katibu Mkuu Chongolo aliwataka viongozi wa CCM kuwafukuza wanachama wanaokisaliti hususani wakati wa uchaguzi, huku akitaka wasichaguliwe viongozi wanaotoa rushwa, kutaka utukufu na sifa kwa manufaa binafsi.

Chongolo aliyeko mkoani humo kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi 2020, alisema: "Viongozi mnapowabaini wasaliti, wafukuzeni, msaliti akifukuzwa hawezi kurudishwa tena ndani ya chama kwa sababu hawezi kuacha hiyo tabia," alisema Chongolo.

Alitolea mfano Uchaguzi Mkuu wa 2020 wananchi wa Hai walikosa jimbo hilo kwa sababu ya usaliti wa wanachama waliamua mgombea akose na chama kikose."Mnatakiwa kuacha nongwa na kusalitiana na uongozi ndani ya CCM ni nafasi za kuachiana na siyo kufanyiana nongwa. Usaliti ni dhambi kubwa," Chongolo alionya.

Alisema wakati wa kampeni za uchaguzi wa 2020, wanachama walionyesha matumaini makubwa ya ushindi katika uchaguzi huo lakini kilichotokea kilimshangaza. Aliwahimiza wasichague aina hiyo ya viongozi ambao lengo lao ni kujinufaisha binafsi na siyo kuwatumikia wananchi katika uchaguzi wa ndani ya chama ngazi ya kata na kuendelea hadi ngazi ya kitaifa.

Alisema waangalie watu ambao wana msukumo wa kutumikia wananchi kwa moyo na kujituma na siyo wanaosukumwa na mambo mengine.

"Mungu ndiye anayepanga nani awe kiongozi na siyo vinginevyo, chama hiki ni cha wote na siyo cha watu warefu wala wafupi ambao wataonekana wanastahili kuchaguliwa, hivyo msikosee kuchagua viongozi," alitahadharisha.

***Imeandikwa na Augusta Njoji (DODOMA) na Mary Geofrey (HAI)**

# 2,900 mbaroni tuhuma za uhamiaji haramu

**Na Restuta Damian,**
BUKOBA

IDARA ya Uhamiaji mkoani Kagera imewakamata watu 2,935 wanaodaiwa ni wahamiaji haramu kutoka mataifa mbalimbali kufuatia msako maalum uliofanywa kuanzia Januari hadi Juni mwaka huu.

Watu hao wanadaiwa wanatoka nchi za Rwanda, Kenya, Congo (DRC), Zimbabwe, Ethiopia, Somalia, China, Burundi, Uganda na Zambia.

Mkuu wa Idara ya Uhamiaji Mkoa wa Kagera, Thomas Fussy, alibainisha kukamatwa kwa watuhumiwa hao alipozungumza na Nipashe jana kuhusu tatizo la uhamiaji haramu mkoani humo.

Fussy alisema kati ya watuhumiwa hao, 2,735 waliondolewa nchini huku wengine 183 wakifikishwa mahakamani na 22 walipewa vibali vya ukazi.

Alisema kati ya Januari hadi Juni mwaka huu, ofisi yake ilifanya msako ili kuhakikisha raia wa mkoa huo wanakuwa salama.

Kutokana na hatua hiyo, Fussy aliwaomba watendaji wa mitaa, vijiji na kata mkoani Kagera kuhakiki taarifa za wananchi wanaofika ofisini kwao kuomba barua za utambulisho wa ukazi wa maeneo yao.

Alisema mkoa huo unapakana na nchi za Rwanda, Uganda na Burundi na kwamba ofisi yake ilifanya msako na kubaini baadhi ya nyaraka zinazotolewa na watendaji wa serikali za mitaa, vijiji na kata zinawatambulisha wahamiaji haramu kuwa ni wakazi wa eneo lao.


Alisema idara hiyo imebaini mkoa una idadi kubwa ya wahamiaji walowezi (wageni wasiohamishika) na kwamba wanataka kuanza kuwapa vibali maalum ambavyo vinatolewa kwa njia ya kielektroniki ili kuwatambua.

"Hivi vibali vinatolewa kwa wale ambao waliingia tangu miaka ya 70 waliokuja kama wageni na kuishi muda mrefu zaidi ya miaka 20," alisema Fussy.

Alisema wahamiaji hao huingia nchini kwa kujipenyeza na kuanza kuomba vitambulisho na kadi za kupigia kura bila kufuata taratibu zinazotakiwa kisheria.

Pia alisema kuna wahamiaji haramu ambao wanaingia nchini kupitia mipaka ya mkoa huo na kuanza kujishughulisha na shughuli za kilimo na ufugaji.

"Wahamiaji hawa wanakuja na mambo mengi yenye madhara ambayo yanasababisha mmomonyoko wa maadili kwa jamii ambayo wanaishi nayo na kushirikiana katika shughuli mbalimbali bila kujuana," alisema Fussy.



Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Angel Akilimali (kulia), akimkabidhi diski mweko yenye mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Huduma za Habari ya 2016 kwa Mhariri Mtendaji wa gazeti la The Guardian, Wallece Mauggo (kushoto) na Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, alipotembelea chumba cha habari cha Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), Mikocheni, Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vyombo vya habari vyataka sheria rafiki

**Na Jenifer Gilla**

UIMARA wa vyombo vya habari nchini utatokana na kuundwa kwa sheria rafiki, zisizo na vitisho, kukandamiza na kunyanyapaa wanahabari.

Kauli hiyo imetolewa na Mjumbe wa Kamati Tendaji ya Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Angela Akilimali, jana alipotembelea ofisi za magazeti ya The Guardian na Nipashe ikiwa moja ya ziara ya kukusanya maoni kutoka kwenye vyombo vya habari ya kuboresha sheria hizo.

Alisema mchakato wa mabadiliko ya sheria za vyombo vya habari nchini, unalenga kujenga mazingira rafiki na bora kwa wanahabari wakati wa kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Akilimali alisema, sheria zilizopo sasa zinakinzana na malengo ya ukuaji wa tasnia ya habari nchini, pia chanzo cha kudumaza tasnia hiyo.

"Yapo mabadiliko mengi yaliyofanywa mwaka 2016, kwenye Sheria ya Huduma za Habari yanayokinzana na kukua kwa tasnia hii, mfano huwezi kuunda Bodi ya Ithibati halafu serikali iisimamie bodi hiyo.

"Wanahabari kama taaluma nyingine ina watu wenye weledi wa kutosha hivyo badala ya kuwa na vyombo vingi kama vilivyotajwa kwenye sheria hii (Bodi ya Ithibati, Mfuko wa Mafunzo na Baraza Huru la Vyombo vya Habari), tunaona tuwe na chombo kimoja tu ambacho ni Baraza Huru la Vyombo vya Habari ili kusimamia mambo yote ya wanahabari na tasnia kwa ujumla," alisema Angela.

Alitaja kikwazo kingine kwenye tasnia ya habari ni sheria kulazimisha chombo cha habari hususani magazeti kuomba leseni kila mwaka jambo ambalo linasababisha usumbufu mkubwa.

"Hatuoni sababu kwa vyombo vya habari hususani magazeti kuwekewa utaratibu wa kukata leseni kila mwaka, kama ilivyokuwa awali kabla ya mabadiliko ya 2016 kwamba usajili ni mara moja, utaratibu huu unafaa kuendelea," alisema Angela.

Aidha, alisema tasnia ya habari inahitaji uwekezaji mkubwa, kuweka mipaka ya uwekezaji kwa wageni kutoka nje kama inavyoelekeza sheria, kunaua tasnia hiyo.

"Kwenye hii sheria yapo mambo mengi magumu, lipo hili la kulazimisha mwekezaji kutoka nje awe na asilimia isiyozidi 49, lakini tunajiuliza mbona wawekezaji kwenye mitandao ya simu wanawekeza kwa asilimia 100 na wao wana wateja zaidi ya milioni 10.

"Kwanini tasnia ya habari wazuiwe, hii tunasema hapana. Tunasema hivyo kwa kuwa uwekezaji kwenye habari unahitaji mtaji, hivyo kama ilivyo uwekezaji mwingine, kwenye habari akiwamo mwekezaji anayetaka kuwekeza kwa asilimia 100, aruhusiwe," alisema.

Wallace Maugo, Mhariri wa Gazeti la The Guardian alisema wanahabari wanapaswa kuwa pamoja katika kuhakikisha sheria zinazominya uhuru wa habari na wanahabari zinabadilishwa.

Alisema mchakato wa mabadiliko haya umeanza wakati muafaka kwa kuwa, Rais aliyepo madarakani Samia Suluhu Hassan ni msikivu katika mambo mbalimbali.

"Tunapaswa kuwa pamoja wanahabari wote, lakini tuna bahati nzuri maana katika mchakato huu Rais ni msikivu kabisa na anaonekana kuwa na dhamira ya kweli," alisema Maugo.

James Marenga ambaye ni Wakili wa Kujitegemea alisema vyombo vya habari nchini kwa sasa vinaweza kukosoa tofauti na miaka mitano ama sita iliyopita, lakini tatizo lililopo ni kwamba kukosoa huko hakulindwi kisheria.

Marenga ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA-TAN), alisema kwa sasa vyombo vya habari nchini vinaandika na hata kukukosoa, lakini pale mwandishi ama chombo cha habari kinapowindwa, sheria zilizopo zinatumika.

"Mwandishi anaweza kufungwa kwa sheria zile zile ama chombo cha habari kinaweza kuondolewa sokoni kwa sheria hizo hizo, ndiyo maana tunasema uhuru wa habari lazima ulindwe kisheria," alisema Wakili Marenga.

Alisema kuwapo kwa sheria za habari kwa kiwango kikubwa kumesababisha kushuka kwa habari za uchunguzi, na baadhi ya wanahabari wamepoteza vifaa vyao kutokana na polisi kuvitwaa kwa ajili ya upekuzi.

"Sheria hii imewapa mamlaka makubwa polisi, wanapoamua kukufuatilia na hata kuchukua vifaa vyako, wanaweza kufanya hivyo kwa sheria hii. Kwa nchi ya Ghana lazima polisi awe na kibali, lakini hapa kwetu hiyo haipo," alisema.

## Rais Samia kufungua Kongamano la Nishati

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajia kufungua Kongamano la Nne la Nishati Tanzania 2022 leo linalodhaminiwa na PanAfrican Energy Tanzania.

Kaulimbiu ya kongamano hilo linalofanyika kwa siku mbili kuanzia leo ni 'Awamu Inayofuata katika Sekta ya Nishati Tanzania: Kukuza Uwekezaji na Ukuaji'.

Akizungumzia kongamano hilo jana, Mkurugenzi Mkuu wa PAET, Andrew Hanna, alisema: "Tuna furaha kubwa kuhusu kongamano hili litakaloleta mwelekeo kwenye sekta hii nchini.

"Ni fursa nzuri ya kupata muda na wasimamizi pamoja na serikali kubadilishana mawazo kuhusu Sekta ya Nishati na kile kinachohitajika ili kuhakikisha uhakika wa uzalishaji kwenda mbele, ili kukidhi ongezeko la mahitaji ya gesi katika uchumi wa viwanda wenye mafanikio makubwa."

Alisema Orca Energy Group ni kampuni mama ya PAET, inaendelea kuwekeza katika shughuli zake za Songo Songo ili kuendana na ukuaji wa Tanzania katika uzalishaji wa umeme na upanuzi wa viwanda.

Alisema katika miaka miwili iliyopita, kampuni imewekeza zaidi ya dola za Marekani milioni 70, katika kuongeza na kuendeleza usambazaji wa gesi, ikiwa ni pamoja na dola za Marekani milioni 42.5 katika mradi wa ukandamizaji wa gesi katika kiwanda cha kuchakata gesi kinachomilikiwa na Songas ambacho kinaendeshwa na PAET, na zaidi ya dola za Marekani milioni 31.6 zilizowekezwa kukarabati visima vitatu.

Alisema Mhandisi wa PAET, Revocatus Kasheshi, atatoa mada maalumu ya kielimu kuhusu usimamizi wa hifadhi zilizokomaa kwa kutumia uzoefu wa miaka 18 iliyopatikana katika uzalishaji wa gesi Songo Songo.

Alisema, kampuni pia itakuwa na banda la maonyesho kwa muda wote wa kongamano ili kuwapa wageni fursa ya kuzifahamu shughuli zinazohusu PAET kama mzalishaji wa kwanza wa gesi nchini na michango yake kwa uchumi wa Taifa - moja kwa moja na kwa njia isiyo ya moja kwa moja.

## Ahukumiwa miaka 10 jela kujaribu kumuua mtalaka wake

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza, imemhukumu William Hamisi (49), kifungo cha miaka 10 jela kwa kosa la kujaribu kumuua mtalaka wake, Mirembe Isomelo kwa kumchoma kisu tumboni na utumbo kutoka nje.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani mbele ya Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, John Kahyoza na aliposomewa shtaka lake alikiri kosa kwa madai kuwa alimkuta mtalaka wake na mwanaume mwingine chumbani.

Awali, Wakili wa Serikali, James Pallangyo, alidai mahakamani kuwa mshtakiwa na mke wake walibahatika kupata watoto wawili na kwa muda mrefu ndoa yao haikuwa na furaha.

Pallangyo alidai kuwa Juni 16, 2015, Isomelo aliamua kuachana na mshtakiwa na kwenda kuishi kwao, lakini mshtakiwa hakukubaliana na jambo hilo.

Alidai Agosti 14, 2015 usiku, mashtakiwa alikwenda kwa mtalaka wake na kuvunja mlango wa chumba alimokuwa amelala mtalaka wake na kumkuta na mwanaume mwingine na kufanya jaribio hilo kwa kumchoma kisu tumboni.

Aliendelea kudai kuwa mwanamke huyo alipiga kelele na mama yake mzazi alipoenda, mshtakiwa alikimbia lakini alikamatwa na majirani.

Aidha, alidai mshtakiwa alipohojiwa na polisi alikiri kumchoma kisu mtalaka wake kwa sababu ya wivu wa mapenzi.

Jaji Kahyoza akitoa hukumu alisema: "Mahakama hii imekutia hatiani kwa kukiri kosa lako la kujaribu kumuua mtalaka wako Mirembe Isomelo kwa kumchoma kisu tumboni."

Alipotakiwa kujitetea, kupitia Wakili wa Kujitegemea Penina Mashimba, alidai kuwa mteja wake ni mkosaji wa kwanza na amejutia kosa lake ndiyo maana amekiri kosa bila kulazimishwa.

Pia, mteja wake alikaa mahabusu miaka sita na miezi 11 amejifunza, na kuiomba mahakama hiyo impe adhabu ndogo ya kifungo cha nje.

Hata hivyo, Wakili wa Serikali, Pallangyo aliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa huyo kwa kuwa ukatili wa kisingizio cha wivu wa mapenzi umekithiri Kanda ya Ziwa na kwamba akiadhibiwa itakuwa fundisho kwake na wanaume wengine.

Jaji Kahyoza alisema kumchoma mwanamke kisu tumboni hadi utumbo kutoka ikizingatiwa kuwa alikuwa ameachana naye ni kitendo cha kikatili.

"Nakuhukumu kwenda jela miaka 10 na Jeshi la Magereza likupunguzie miaka uliyokaa mahabusu gerezani, rufaa ipo wazi kwa upande wowote ambao haujaridhika na hukumu hii," alisema Jaji huyo.

# Watalii wamiminika nchini

**Na Romana Mallya**

FILAMU ya The Royal Tour imeendelea kuleta neema Tanzania baada ya abiria 845, kushuka kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA).

Kwa mujibu wa taarifa ya Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa aliyoandika kwenye ukurasa wake wa Instagram, juzi usiku Shirika la Ndege la KLM la Uholanzi lilishusha abiria zaidi ya 250. "Kwa kweli kishindo ambacho Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amekisababisha katika sekta ya utalii kikubwa sana," sehemu ya taarifa hiyo ilisema.

Msigwa alisema jana ndege zilizoshusha abiria na idadi yake kwenye mabano ni Ethiopia Airline (355), Qatar Airways (240) na KLM (250).

Julai 14, mwaka huu, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ilitoa takwimu za watalii waliongia nchini katika kipindi cha Januari hadi Mei, 2022, ikionyesha ilifikia idadi ya 458,048 ikilinganishwa na 317,270 walioingia nchini kipindi kama hicho mwaka 2021.

Kaimu Mkurugenzi za Takwimu za Uchumi kutoka NBS, Daniel Masolwa alisema idadi hiyo ni ongezeko la watalii 140,778 sawa na asilimia 44.4.

Alisema kati ya watalii 458,048 walioingia nchini mwaka huu, 137,758 wameingia kupitia Zanzibar ambao ni sawa na asilimia 30.1 ya wageni wote.

"Watalii walioingia nchini mwezi Mei pekee waliongezeka hadi 89,271 ikilinganishwa na 42,173 walioingia mwezi Mei, mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 117.7.

Aprili 28, mwaka huu, Rais Samia alizindua filamu ya Royal Tour kwa lengo la kutangaza utalii wa Tanzania kimataifa na kuvutia wawekezaji kuja kuwekeza maeneo tofauti na kukuza uchumi.

Katika bajeti ya mwaka 2022/23, Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Pindi Chana, alisema serikali imepanga kutekeleza mpango wa kuimarisha sekta ya utalii kwa kuongeza idadi ya watalii kufikia milioni tano na kupata mapato ya Dola za Marekani bilioni sita ifikapo 2025.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Ramadhan Ng'anzi (kulia), akimsikiliza Mkuu wa Kitengo cha Wateja wa Benki ya Afrika, Ninael Mndeme, alipofanya ziara ya kikazi ofisini kwake, jijini Mwanza juzi, akiongoza ujumbe wa maofisa wengine wa benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bashungwa awapa maelekezo ma-RC

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imewataka wakuu wa mikoa kuhakikisha wakurugenzi wa halmashauri wanawalipa wanaokusanya mapato kwa wakati na fedha zinazokusanywa zinakwenda benki ili kuondoa mianya ya upotevu wa mapato.

Pia yeyote anayecheza na mifumo ya ukusanyaji mapato achukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria na sio vinginevyo.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, wakati akitoa taarifa ya mapato na matumizi ndani ya halmashauri kwa mwaka 2021/22 lengo likiwa ni kuongeza la uwazi na uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato.

Alisema zipo baadhi ya halmashauri mfano ya wilaya za Kilosa na Kiteto ambazo kwa mujibu wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2020/21, hazikuhuisha leseni za biashara hali iliyosababisha kukosa mapato.

Bashungwa aliwataka wakuu wa mikoa wahakikishe makisio ya bajeti za mapato ya ndani ya halmashauri zinazingatia uhalisia wa vyanzo vya mapato ili kuwa na matokeo halisi.

"Zipo halmashauri ambazo zimekusanya zaidi ya asilimia 100, lakini hazikuwahi kuomba kuhuisha bajeti zao ziendane na uhalisia kama vile halmashauri za wilaya za Kibaha, Mlele na Halmashauri ya Mji wa Mbulu," alisema. Alizitaka halmashauri zote zitekeleze mapendekezo na kufunga hoja zote za ukaguzi zilizotolewa na CAG.

Pia aliagiza halmashauri zihakikishe fedha zilizovuka mwaka wa fedha 2021/22 (Bakaa) zinatumika kabla ya Septemba 30, mwaka huu kwa kufuata sheria, kanuni, taratibu na miongozo.

Alitaka kufanyike ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwenye ngazi za kata na kudhibiti matumizi mabaya ya fedha zinazotoka serikali kuu na fedha za mapato ya ndani zinazoelekezwa kwenye ngazi ya kata ili zielekezwe kwenye miradi yenye tija kwa wananchi.

Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha imeongoza katika halmashauri zote kwa kukusanya asilimia 247 ya makisio yake ya mwaka, ikifuatiwa na halmashauri za wilaya ya Mlele asilimia 185 na Morogoro asilimia 158.

Bashungwa alisema ongezeko hilo limetokana na Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha kufanya mauzo ya eneo la uwekezaji, ambayo hayakuwa sehemu ya bajeti ya halmashauri hiyo.

Alisema kumekuwa na ongezeko la ushuru wa huduma kutoka Bwawa la Mwalimu Nyerere kwa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro na Rufiji.

Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli imekuwa ya mwisho kwa kukusanya asilimia 58 ya makisio yake ya mwaka, ikifuatiwa na Korogwe asilimia 67 na Bunda asilimia 70 ya makisio yake ya mwaka.

Halmashauri nne zimekusanya chini ya Shilingi bilioni moja ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli ambayo imekuwa ya mwisho kwa kukusanya Sh. milioni 599.7, ikifuatiwa na Kigoma Sh. milioni 692.1, Madaba Sh. milioni 792.3 na Buhigwe Sh. milioni 880.2.

Alisema uchambuzi wa taarifa za mapato kwa kuzingatia ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ya halmashauri kimkoa, unaonyesha Mkoa wa Pwani umeongoza kwa kukusanya asilimia 118 ya lengo la mwaka, ikifuatiwa na Mkoa wa Manyara asilimia 114, Katavi (112), Songwe (111). Lindi umekua wa mwisho kwa kukusanya asilimia 87, ukifuatiwa na mikoa ya Mtwara na Geita (93).

Bashungwa alisema kwa kuzingatia wingi wa mapato (pato ghafi), Mkoa wa Dar es Salaam umekusanya mapato mengi zaidi kuliko mikoa mingine, kwa kukusanya Sh. bilioni 167.5 ikifuatiwa na Mkoa wa Dodoma Sh. bilioni 89.4 na Mkoa wa Pwani Sh. bilioni 48.7.

Alisema Mkoa wa Rukwa umekuwa wa mwisho kwa kukusanya Sh. bilioni 9.4 ukifuatiwa na Mkoa wa Katavi kwa kukusanya Sh. bilioni 13.6 na Mkoa wa Simiyu Sh. bilioni 14.

Aidha, alisema TAMISEMI imeanza kuchukua hatua kama kuwabadilisha vituo baadhi ya wakuu wa idara na vitengo, kufanya msawazo kwa watumishi na kuwabadilishia majukumu baadhi ya wakuu wa idara na vitengo kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi na kuondoa utendaji kazi wa mazoea.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Wazazi msimwache nyuma mtoto wa kike masomo sayansi

**IPO** dhana kwenye jamii kuwa mtoto wa kike au mwanamke sio wa kusoma au kufanyakazi ngumu badala yake zinapaswa kufanywa na mtoto wa kiume jambo linalorudisha nyuma au kuua ndoto zao.

Kwa muda mrefu Tanzania imeweka mikakati ya kuongeza na kushawishi watoto kupenda masomo ya sayansi ikiwamo kutoa zawadi, ufadhili wa masomo na mikopo ya elimu ya juu kwa asilimia 100.

Kuwavunja moyo watoto wa kike kuchukua masomo hayo kumesababisha fani za taaluma hiyo kuchukuliwa na watoto wa kiume.

Ukiangalia marubani wengi wa ndege, marubani wa meli, wahandisi na fani zenye taaluma ya masomo ya sayansi wanawake ni wachache sana ikilinganishwa na wanaume.

Hata inapotokea mtoto wa kike kuwa rubani wa meli au chombo ambacho kimezoeleka kuendeshwa na mwanaume inaonekana kuwa jambo lisilo la kawaida.

Unapotembelea vyuo vikuu utabaini kukosekana kwa wanawake wengi wanaosoma masomo ya sayansi, hali ambayo ilisukuma serikali na wadau kuweka nguvu ili kuwapa motisha.

Pia, wanawake wanaohitimu vyuo vikuu katika fani za sayansi wameajiriwa kwa haraka, lengo ni kutoa motisha zaidi na tayari tunaona mafanikio ya ongezeko la madaktari kwenye jamii.

Hivi karibuni Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitangaza kuanza kutoa ufadhili kwa wanafunzi waliofaulu masomo ya sayansi ikiwa wataendelea na masomo hayo ngazi ya chuo kikuu, ambao watasoma bure kwa vyuo vya ndani na unaangaliwa uwezekano wa kuwapeleka nje ya nchi.

Wakati jitihada hizo za wadau zikiendelea bado kwenye jamii yetu kuna mtazamo hasi dhidi ya watoto wa kike kusoma masomo ya sayansi, hali hiyo huanzia ndani ya familia kwa kuwaaminisha ni magumu.

Lakini mazingira ya shule nayo huwakatisha tamaa kwa kuwa hakuna vifaa vya maabara vya kujifunzia kwa vitendo hali inayoongeza ugumu kwao kwa kuwa masomo hayo hueleweka kwa vitendo zaidi.

Julai 31, mwaka huu wadau wa elimu na sayansi nchini walipoadhimisha Siku ya Mwanamke wa Kiafrika pamoja na mambo mengine walisema kuwa malezi yanachangia pia kurudisha nyuma ndoto kusoma sayansi.

Tunatoa angalizo kwa wazazi kuacha kulea watoto wao wa kike kizamani bali waendane na kasi ya sayansi na teknolojia ambayo inahitaji wataalam zaidi katika sekta ya sayansi bila kubagua jinsia kwa sababu wanaume peke yao hawatoshi.

Tunawasihi wazazi na walezi wawape watoto wao wa kike muda wa kutosha wa kuendeleza vipaji vyao vya kisayansi badala ya kuwabana wafanye kazi ndogo za nyumbani kama vile kuosha vyombo, kufagia na kudeki wakiamini kuwa huo ndiyo msingi pekee wa maisha.


Pia, tunawakumbusha kuchunguza vipaji vya watoto wao wa kike katika sayansi kupitia shughuli mbalimbali kama vile kuchora, kupaka rangi, kutengeneza vitu mbalimbali katika michezo yao na kuviendeleza.

Watoto wanaathiriwa zaidi na maneno yanayotoka kwa watu wao wa karibu, hasa wazazi na walezi kwa kuwa wanawaamini zaidi, kwasababu hiyo wazazi watumie mwanya huo kuwajenga na kuwatia moyo watoto wa kike katika masomo hayo.

Aidha, tunawasihi wadau wa sayansi nchini kuendelea kufanya uchunguzi na kuibua sababu mbalimbali zinazosababisha mwanamke kuachwa nyuma katika sayansi ili zipatiwe ufumbuzi.

Tunawakumbusha pia kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuwa na usawa wa kijinsia katika sayansi ili wanawake wasiachwe nyuma.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wakuu wapya walioapa tumikieni si kujikweza

**KWA** mara nyingine Rais Samia Suluhu ameteua na kuapisha wasaidizi wake kwa ajili ya kuiongoza mikoa, akiwaondoa baadhi yao na wengine kuhamishwa na pia wamo waliobakizwa katika vituo vyao vya kazi.

Katika uteuzi wa viongozi mbalimbali amewahi kusisitiza jambo moja kuwa anataka wafanye kazi kwa ushirikiano na kutoa onyo kuwa hatasita kumwondoa kiongozi yeyote ambaye atainua mabega.

Anawakumbusha kuwa asiwepo kiongozi wa kwenda kinyume na kuanza kuinua mabega yake au kufanya anavyotaka, bali kuwatumikia wananchi katika eneo lake la kazi, ili kuharakisha maendeleo.

Hapa inawezekana anawasisitizia kutambua kuwa cheo ni dhamana, uongozi ni utumishi, hivyo kiongozi asidhani cheo ni matokeo ya jitihada zake binafsi, akiamini anaweza kufanya lolote analotaka.

Kwa mantiki hiyo, si vibaya wakuu wapya wa mikoa walioteuliwa na kuapishwa juzi, wakiwamo waliohamishwa vituo vya kazi, wakazingatia maelekezo hayo ya mkuu wa nchi, ili walete matokeo chanya ya maendeleo katika maeneo yao ya utawala.

Labda nikumbushe kauli ya mwanasiasa aliyewahi kusema cheo ni sawa na koti la kuazima ambalo mtu unakuwa na mbwembwe akiwa amelivaa, lakini siku koti hilo linapochukuliwa, mtu anakosa mahali pa kuficha uso wake.

Kutokana na msemo huo, akawataka viongozi vijana kuelewa kuwa madaraka au vyeo walivyobeba ni kama koti la kuazima na kwamba ipo siku hawatakuwa navyo. Hivyo wawatumikie wananchi.

Anatoa ushauri huo, kutokana na kile alichodai kuwa ameona baadhi ya nyadhifa au vyeo baadhi vya watu wanavichukulia kwa namna wanavyopenda na kutunisha misuli kuwa ni wakubwa.

Ninaamini kwa mfano huo na kile Rais amekuwa akihimiza kwa wataule wake, wanakwenda kutekeleza wajibu wao kikamilifu huku wakikumbuka ahadi za mwanachama hasa ya tano inayokumbusha kuwa 'cheo ni dhamana, sitatumia cheo changu wala cha mtu mwingine kwa faida yangu'.

Kimsingi, kiongozi anayezingatia ahadi hiyo, hawezi kujiinua atakumbuka kuwa cheo ni sawa na koti la kuazima ambalo wakati wowote mwenye nalo anaweza kulichukua.

Aidha, iwapo kiongozi atazingatia ahadi hiyo, atafanya kazi akigusa hata ile ya pili ambayo inamwelekeza kuitumikia nchi na watu wake wote' ili kuharakisha maendeleo.

Sasa kwa kuwa Rais alishasema kiongozi atakayekuwa anafanya apendavyo ataondolewa kwenye nafasi yake, basi ni vyema kila aliyeteuliwa, afanyie kazi ujumbe huo ili 'asisaidiwe kazi' au kutumbuliwa.

Ninaamini kiongozi akitimiza wajibu wake inavyopasa hakutakuwa na mtindo wa kujitwalia madaraka mikononi awapo kwenye kituo chake cha kazi, kwani hatua hiyo inaweza kuwa sawa na kuinua mabega.

Ikumbukwe, kuna wakati baadhi ya wakuu wa wilaya na mikoa waliwahi kusababisha aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Tawala za Mikoa (TAMISEMI), Selemani Jafo, kuingilia kati na kukemea mtindo huo wa kutumia vibaya madaraka kwa kuwaweka watu ndani.

Akafafanua kuwa, Sheria ya TAMISEMI ya Mwaka 1997, Kifungu cha 15 (1) inawapa mamlaka wakuu wa wilaya na mikoa kutoa amri mtu kukamatwa na kuwekwa ndani saa 48 anapobainika mhusika ametenda kosa fulani.

Lakini, akatoa somo kwamba, tabia ya kuweka watu ndani ovyo, inasababisha wananchi waichukie serikali na kuwaagiza wakuu hao kuitumia sheria hiyo kama ilivyokusudiwa na si kwa kuonea watu.

Viongozi wasisubiri mpaka Rais au Waziri Mkuu atembelee eneo lao ndipo washtakiwe kwa mabango kuwa wameshindwa kumaliza kero za wananchi badala yake wajitume na kuwafikia wananchi na kushirikiana nao ili kuwaletea maendeleo.

## Unyonyeshaji watoto wachanga waongezeka

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Khamisi, amesema unyonyeshaji wa watoto wachanga ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa umeongezeka kufikia asilimia 90 ikilinganishwa na asilimia 54 ya mwaka 2018.

Alikuwa akizungumza wakati wa uzinduzi wa maadhimisho ya wiki ya unyonyeshaji maziwa ya mama kitaifa iliyofanyika Halmashauri ya Ikungi, mkoani Singida.

Alisema utoaji vitamin A kwa watoto wa miezi sita hadi 59 umeongezeka kwa asilimia 64 hadi 97 kwa miaka hiyo.

Hata hivyo, alisema kuwa asilimia 43 ya watoto hunyonyeshwa kwa miaka miwili na kuendelea huku asilimia 57 hunyonyeshwa maziwa ya mama pekee bila kuchanganya na chakula kingine kwa miezi sita.

"Utafiti unaeleza kuwa mtoto akizaliwa na kuanza kunyonyeshwa maziwa ya mama ndani ya saa moja kunaweza kuokoa uhai wake kwani kuchelewa kumnyonyesha kunachangia kwa kiasi kikubwa vifo vya watoto wachanga ndani ya siku 28," alisema Waziri Mwanaidi.Alisema pia asilimia 97 ya watoto wanaozaliwa hunyonyeshwa maziwa ya mama na asilimia 92 ya watoto hunyonyeshwa kwa mwaka mmoja na kuendelea.

Aliwahimiza wahudumu katika vituo vya kutolea huduma za afya kutoa huduma kwa wakati husika na kuwataka wazazi kuendelea kuhudumia kliniki kama inavyoagizwa.

Aliwasihi wazazi kuwanyonyesha watoto wachanga maziwa ya mama pekee kwa kipindi cha miezi sita na kuwanyonyesha watoto hao kwa miaka miwili na zaidi.

"Kunyonyesha maziwa ya mama kuna faida nyingi kwa mama na mtoto kwa kuwa kunaimarisha afya na ustawi wa mama na mtoto. Vilevile huzuia aina zote za utapiamlo kwa kuwa kunakuwa na uhakika wa chakula kwa watoto wachanga na wadogo," alifafanua.

Alisema pia unyonyeshaji ukifanyika ipasavyo, familia jamii na taifa wanapata faida nyingi, ikiwamo watoto kuwa na lishe bora itakayoboresha ukuaji na maendeleo ya kimwili na kiakili kwa kuwa watakingwa dhidi ya magonjwa na kupunguza vifo vya watoto nchini.

Alisema maadhimisho hayo yanakumbusha umuhimu wa kuboresha lishe ya watoto kwa kutekeleza utaratibu sahihi wa unyonyeshaji wa maziwa ya mama ili kujenga msingi imara wa afya na uhai wa watoto ambao ni taifa la kesho.

Mwaka 2018 baraza la afya ambalo ni bodi ya kufanya uamuzi katika Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), liliidhinisha wiki ya unyonyeshaji duniani, Agosti 1 -7, kila mwaka kama mkakati muhimu wa kukuza unyonyeshaji.

Kwa mujibu wa WHO, kati ya watoto watano, watatu hawanyonyeshwi ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa wakati maisha ya watoto zaidi ya 820,000 chini ya miaka mitano yanaweza kuokolewa ikiwa watoto wote wa miezi 0 mpaka 23 watanyonyeshwa kikamilifu.

# Shule zakabiliwa na uhaba wa madawati

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

SHULE za msingi zilizoko katika Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza, zinakabiliwa na uhaba wa madawati 4,000 kati ya 5,838 yanayohitajika kwa sasa.

Kutokana na hatua hiyo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Hassan Massala, amechukua hatua za haraka ili kuwanusuru wanafunzi kukaa chini, akifanikiwa kupata madawati 1,525.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi madawati hayo kwenye shule hizo iliyofanyika wilayani humo jana, Massala alisema wakati wanaendelea na ujenzi wa madarasa, waliona waongeze kasi katika sehemu ambayo watoto watakaa ili wapate haki yao ya msingi ya kupata elimu katika mazingira bora.

Alisema kutokana na takwimu hizo, waliona wana wajibu wa kufanya jitihada za makusudi ili kukabiliana na uhaba huo wa madawati ikiwamo kuwashirikisha wadau kwa lengo la kupata madawati 1,525.

"Tulifanikiwa kukusanya fedha na madawati ambapo jumla ya vyote hivyo ni madawati zaidi ya 2,000, mpaka leo (jana) tunapozungumza tumefanikiwa kutengeneza madawati 1,525 ambayo tumetumia Sh. milioni 100. Kwa sababu fedha tulichangisha hadharani na madawati tumeona tuyagawe hadharani.

"Tumewaita watoto ambao wanakaa watatu watatu na ndivyo inavyopaswa (kisera). Kabla ya hapo, watoto hao wakiingia kwenye madarasa wakati mwingine walikaa wanne au watano kwenye dawati moja na wengine wanakaa chini," alisema Massala.

Alisema baada ya kupata madawati hayo, bado watakuwa na uhaba wa mengine 4,000 na wamejiwekea lengo kufikia Juni 2023 wawe wamemaliza upungufu huo.

"Ili tujenge Ilemela na ili tujenge Mwanza na taifa ambalo lina watu wenye uelewa na maono, lazima tuwekeze kwao na lazima tuanze kuwekeza, leo tumewakusanya hapa ili tushuhudie tulichojaribu kukifanya wote kama watu wa Ilemela," alisema.

Mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Msingi Buswelu, Juliana Anthony, aliahidi kusoma kwa bidii na kutimiza malengo yake kwa kuwa wamesaidia madawati ambayo yatawafanya wasome katika mazingira mazuri.

Meneja wa Benki ya Stanbic Tawi la Mwanza, Geofrey Makondo, alimpongeza Mkuu wa Wilaya ya Ilemela kwa maono na usimamizi wake ambao umefanikisha watoto kupata madawati.

"Ninaamini watoto hawa kwa kupata madawati watasoma vizuri na uelewa utaimarika, kwenye takwimu bado tuna upungufu wa madawati, vyumba vya madarasa na nyumba za walimu, wadau wenzangu niombe tuendelee kujitolea," alihimiza.




Ofisa wa Benki ya NBC, akitoa ufafanuzi kuhusu huduma zinazotolewa na benki hiyo, kwa wadau mbalimbali waliotembelea banda la maonyesho ya kilimo la benki hiyo, katika maonyesho ya Kilimo Nanenane katika viwanja wa John Mwakangale jijini Mbeya jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Malezi kikwazo wanawake katika masomo ya sayansi

**Na Jenifer Gilla**

MKURUGENZI wa Asasi ya Utu na Mazingira, Sarah Pima, amesema mfumo wa malezi una mchango mkubwa katika kupunguza idadi ya watoto wa kike wanaosoma masomo ya sayansi na wataalamu kwenye sekta hiyo.

Alitaja visababishi kuwa ni malezi, mifumo ya maisha, mila na desturi ambazo zinapaswa kuachwa ili kuwashawishi watoto kupenda masomo hayo.

Akizungumza wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mwanamke wa Kiafrika waliyoiandaa kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), Wakala wa Ushirikiano wa Kimataifa wa Maendeleo wa Sweden (SIDA) na Taasisi ya Women Level Up, alisema bila kuondokana na vikwazo hivyo bado kuna safari ndefu.

Alisema lengo la maadhimisho hayo ni kuhamasisha ushiriki sawa kwenye sayansi ili kuongeza idadi ya wanawake katika sekta hiyo, pamoja na kuelimisha wazazi kulea watoto wa kike kisayansi, wanapokuwa wakubwa wasione ngumu.

"Wanawake wengi na vijana wameishia ndoto zao za kisayansi katikati kutokana na malezi. Kuanzia nyumbani mtoto wa kike anaambiwa kuwa masomo ya udaktari ni kazi ya kiume, mwanamke anakuwa nesi, sasa kama mtoto alikuwa na hiyo ndoto inakufa hapo hapo," alibainisha Sarah.

Aidha, alisema kuwa jitihada za pamoja kati ya serikali na wadau wa elimu na sayansi zinahitajika ili kuhamasisha wanawake kupenda masomo ya sayansi kwa sababu wameachwa nyuma licha ya kuwa wanaopokuwa shuleni wanayasoma masomo hayo.

"Katika elimu ya sekondari wanawake wanaosoma sayansi wanakuwa wengi, lakini kadri ngazi ya elimu inavyopanda wanapungua mpaka inapofika kwenye ajira wanazidi kupungua zaidi. Kwa hiyo tuendelee kukaa kwa pamoja kutafuta suluhisho sahihi kwa kushirikiana na serikali ili mwanamke asiachwe nyuma.

Vilevile, Sarah alisema maadhimisho hayo yanalenga kuunga juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan kuhimiza wanawake kujiendeleza kwenye masomo ya sayansi, ikiwamo kujenga shule hizo ngazi ya halmashauri.

Naye Ofisa wa Programu ya Sayansi, Asilia Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), Keven Robert, alisema wameshiriki katika maadhimisho hayo ili kutambua na kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika uchumi kupitia sayansi.

Aliongeza kuwa UNESCO inaamini katika ajenda ya kuhamashisha ushiriki wa mwanamke na watoto wa kike na vijana katika sayansi, teknolojia na ubunifu na hushirikiana na taasisi nyingine katika shughuli zote zinazolenga kumwinua mwanamke katika sayansi na uchumi.

"Utafiti za kisayansi ukifanyika matokeo yake yanaleta faida kwa nchi, kwa maana ya kwamba matokeo ya utafiti yanaleta mbinu mpya ambayo ukiuza au kulifanyia kazi unaweza kupata rasilimali au kuongeza mpya," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Mwanamke Initiative Foundation, Wanu Hafidh Ameir, alisema kuwa siku hiyo ni muhimu kwa sababu inatoa nafasi kwa vijana wa kike waliofanikiwa katika sayansi kuwashawishi wenzao kupitia ushuhuda wanaoutoa.

# Waliotuhumiwa sio raia Tanzania, waachiwa huru

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imewaachia huru vijana saba waliotuhumiwa kuwa sio raia wa Tanzania, baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) kuwasilisha mahakamani nia ya kutokuendelea kuwashtaki.

Vijana hao ni Hasafu Amos, Herison Jackson, Richard Lucas, David Musa, Silvester Ruvugo, Koloe Mtula na James Likongaa, ambao walikuwa wakituhumiwa kuingia na kuishi nchini bila kibali.

Mahakama hiyo ilifikia hatua hiyo jana, baada ya Wakili wa Serikali kutoka Idara ya Uhamiaji, Khadija Masoud, kudai mbele ya Hakimu Mkazi Kisutu, Evodia Kyaruzi kuwa DPP amewasilisha hati hiyo kwa washtakiwa saba kati ya 15.

Masoud alidai kesi hiyo ililetwa kwa ajili ya washtakiwa kusomewa hoja za awali, lakini DPP hana nia ya kuendelea na mashtaka dhidi ya washtakiwa hao.

Washtakiwa hao walikuwa wakidaiwa kuwa Raia wa Burundi na walikuwa wakikabiliwa na mashtaka mawili ya kuingia na kuishi nchini bila kibali.

Ilidaiwa walitenda makosa hayo, Machi 30, 2022 wakiwa maeneo tofauti ndani ya Jiji na Mkoa wa Dar es Salaam.

Wakili huyo aliwataja washtakiwa waliobaki katika kesi hiyo ni Justine Sefana, Alex Silvester, Edward Timotheo, Fenias Zakayo, Bonifas Eliface, Hamis Pascal, Mapatano Mathias na Mussa Yosia, hata hivyo, miongoni mwao hawakuwapo mahakamani.

Aliiomba mahakama ipange tarehe nyingine ya kuwasomea hoja za awali. Hakimu Kyaruzi alipanga Agosti 9, 2022 kwa ajili ya kusomewa maelezo hayo.

Pia, alitoa hati za kukamatwa washtakiwa watano ambao hawakuwapo mahakamani na pia hakuna taarifa zozote zilizotolewa na wadhamini wao.



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo (kushoto), akipewa heshima za kimila na Mzee Kimanyi Pankiapo Laiza, baada ya kutembelea mradi wa ujenzi wa kituo cha afya na nyumba za watumishi Chekimaji, Kata ya Masama Rundugai wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: ADAM MZEE**

## DC awataka vijana kujiajiri

**Na Happy Severine,** BARIADI

MKUU wa Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu, Lupakisyo Kapange, amesema hakuna taifa lolote duniani ambalo linaweza kuajiri vijana wake wote katika mfumo rasmi, hivyo ni lazima wengine wakubali kujiajiri.

Amesema kwa karne ya sasa, vijana wanatakiwa kuamka na kufikiri wapi wanaweza kupata fursa za kujiajiri kwenye ajira binafsi ili kujiletea maendeleo.

Kapange alisema hayo jana wakati akizungumza katika ukumbi wa Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO) wilayani hapa katika mafunzo ya vitendo yatakayodumu kwa siku 20 kwa vijana.

Alisema serikali kupitia SIDO imeanzisha mpango wa kusaidia vijana kujifunza kwa vitendo ili wajiajiri, ukitarajiwa kuwanufaisha vijana 103 mkoani Simiyu.

"Kufanya kazi kwa vitendo kunahitaji umakini mkubwa. Ninawataka ninyi vijana mliochaguliwa kwenda kufanya mafunzo hayo, mkaonyeshe uadilifu wa hali ya juu huko mnakopelekwa. Mazoezi haya mnayoenda kufanya yana miiko yake, lazima heshima ikatawale," aliagiza.

Aliongeza kuwa vijana wengi hususani walioko vijijini hawazijui fursa za ajira za kujiajiri zilizopo na kumtaka Meneja wa SIDO kuendelea kuwasaidia ili elimu na ujuzi ufike kwa wengi.

Meneja wa SIDO mkoani Simiyu, Athanas Moshi, alisema serikali inatambua umuhimu wa kuwawezesha vijana kujiajiri na ndiyo maana wameanzisha mpango huo wa kutoa mafunzo kwa vitendo.

Alisema wanafundisha kwa vitendo vijana waliosomea fani mbalimbali na kwamba Simiyu ni miongoni mwa mikoa 12 itakayonufaika na mafunzo hayo.

**Meneja wa SIDO mkoani Simiyu, Athanas Moshi, alisema serikali inatambua umuhimu wa kuwawezesha vijana kujiajiri na ndiyo**

## Barabara ya Boma Ng'ombe – TPC Moshi kujengwa kwa lami

**Na Mary Geofrey,** HAI

SERIKALI imeahidi kujenga barabara ya Boma Ng'ombe hadi TPC Moshi, mkoani Kilimanjaro yenye urefu wa kilomita 25.7 kwa kiwango cha lami.

Ahadi hiyo ilitolewa jana na Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, wakati akizingumza na wananchi wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, akiwa katika ziara ya siku tano mkoani humo ya kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020/25, miradi ya maendeleo na kuhimiza sensa ya watu na makazi itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu.

Awali, Chongolo alipokea malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu tatizo la usumbufu wa barabara hiyo ambayo inategemewa na wananchi pamoja na kutarajiwa kupunguza msongamano kwenye barabara kuu.

"Wakati namuaga Rais kuwa nakuja Moshi nilimshirikisha hili akasema atatoa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wake," alisema Chongolo. Alisema barabara hiyo itavutia wawekezaji ambao wanaenda kutembelea kivutio cha 'maji ya moto' kilichopo wilayani humo na kusaidia kuongeza mapato ya serikali.

Alisema umuhimu wa barabara hiyo pia ni kupunguza msongamano msimu wa mwisho wa mwaka ambao wananchi wa mkoa hurudi kwa wingi nyumbani kutembea.

Aliahidi kuendelea kumkumbusha Rais kuhusu ahadi hiyo ya ujenzi wa barabara ili utekelezaji uanze mapema.

Akiwa kwa Mjumbe wa Shina namba nne eneo la Magadini wilayani humo, Chongolo aliwataka wananchi kuweka akiba ya chakula kutokana na kuwapo uhaba wa mvua mwaka huu nchi nzima hali iliyosababisha mavuno kuwa kidogo.

"Msitumie chakula kidogo mlichovuna kutengenezea pombe bali hifadhini kije kuwasaidia siku za usoni kukitokea uhaba wa chakula na gharama kuongezeka zaidi," alisema Chongolo.

Awali, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Selemani Mfinga, alimueleza Chongolo kuwa, wananchi hao wamekumbwa na ukame mkubwa hali ambayo inatishia kuwapo na njaa kwa siku za usoni.

Naye Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi, aliwahimiza wananchi wa wilaya hiyo kujitokeza kushiriki sensa ya watu na makazi, kujikinga na UVIKO-19 kwa kujitokeza kupata chanjo zinazopatikana kwenye vituo mbalimbali vya afya.

## Wasafirishaji mkaa waomba kupunguziwa ushuru

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WASAFIRISHAJI na wauzaji wa mkaa kwa usafiri wa pikipiki maarufu busta, wameiomba serikali kuwapunguzia mlolongo wa ushuru ili waweze kubeba mkaa kwa ujazo unaotakiwa.

Wamebainisha hayo jana mjini Mlandizi walipokuwa katika kikao cha pamoja na Jeshi la Polisi, Wilaya ya Kipolisi Mlandizi, Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) Wilaya ya Kibaha, watoa huduma za kibenki kutoka NMB na maofisa kutoka kitengo cha Maendeleo ya Jamii.

Katika kikao hicho kilichoandaliwa na TFS wilaya ya Kibaha, Katibu wa kikundi hicho cha wasafirishaji na wauzaji wa mkaa, Ramadhani Rajab, alisema wanapakia magunia yenye ujazo mkubwa ili waweze kupata faida katika biashara yao kutokana na ushuru mkubwa wanaolipa wakiwa njiani.

"Tunanunua gunia la mkaa kwa Sh. 25,000, tunalipa ushuru wa kijiji Sh. 1,000, ushuru wa maliasili kila kilo moja ya mkaa wanatoza Sh. 250, ushuru wa halmashauri kila gunia Sh. 2,000 hapo mafuta tunaweka Sh. 30,000 na gunia tunaenda kuliuza kwa Sh. 60,000 bila ya kuzidisha ujazo hatupati faida," alisema.

Rajabu pamoja na wenzake waliomba serikali kuingilia kati na kuwapunguzia ushuru ili waweze kunufaika na biashara hiyo ambayo kwa sasa wanaifanya katika wakati mgumu kutokana na kubeba magunia yenye ujazo mkubwa ili wapate faida.

Mhifadhi Misitu Wilaya ya Kibaha, Mkama Kusaga, alisema wameandaa kikao hicho kwa lengo la kutoa elimu kuhusu usalama wa barabarani kwa wasafirishaji hao wa mkaa.

Kusaga alisema wasafirishaji hao walielimishwa namna bora ya usafirishaji na kwamba awali walikuwa wakikwepa kulipa ushuru kwa madai ya kupata hasara, lakini baada ya kufanya kikao cha pamoja hivi karibuni kujadiliana kuhusiana na suala hilo sasa wanapita kwenye njia za mageti ya ukaguzi.

"Baada ya kikao cha pamoja na hawa wasafirishaji maarufu busta ambacho kilifanyika mwaka uliopita, mabadiliko yameonekana kwenye makusanyo ya mwezi Julai ambapo tumefikia Sh. milioni 137 kutoka Sh. milioni 46 ya mwaka wa fedha 2021/2022," alisema Kusaga.

Mhifadhi huyo alisema katika kikao hicho cha juzi wamelazimika kuwaunganisha na Idara ya Maendeleo ya Jamii ili waunde vikundi vitakavyonufaika na mikopo, lakini kwa upande wa taasisi za kifedha wamepewa elimu ya namna ya kutunza fedha zao kwa njia salama.

Hata hivyo, wasafirishaji na wauzaji wa mkaa kwa pikipiki zaidi ya 200 waliobainika kuwa na leseni na bima za vyombo vyao idadi yake haikufika kumi.

Kutokana na hali hiyo Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kipolisi Mlandizi, Julieth Lymo, katika kikao hicho aliwataka kuzingatia sheria na kanuni na ukaguzi wa barabarani utakapofanyika ambao hawana vitu vinavyotakiwa, sheria itachukua mkondo wake.

Wasafirishaji hao walielekezwa namna ya kusafiri salama wakiwa barabarani kubeba mizigo ya kiasi ambayo haitawasababishia ajali wakati wa kuisafirisha.

# DAWASA yakarabati bomba kubwa usiku na mchana

**Na Joseph Mwendapole**

MAFUNDI wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), wanafanyakazi usiku na mchana kukarabati miundombinu ya bomba kubwa la inchi 54 eneo la Mapinga na Kerege Mkoa wa Pwani.

Msimamizi wa zoezi hilo, Meneja Uzalishaji na Usambazaji maji DAWASA, Mhandisi Tyson Mkindi, alisema jana kuwa maboresho hayo ni sehemu ya jitihada za mamlaka kuhakikisha inafikia lengo la kupunguza maji yasiyolipiwa hadi kufikia asilimia 23 ifikapo 2025.

Mhandisi Mkindi alisema kazi ya maboresho inafanyika usiku na mchana ili kuhakikisha uvujaji wa maji unadhibitiwa kwa ufanisi na kwa wakati bila kuathiri upatikanaji wa huduma.

"Kazi inayofanyika kwa eneo la Mapinga kwa Njwaba ni kuondoa kizibo na kufanya maunganisho ya bomba la inchi 54, ambapo kwa sasa kazi imekamilika tayari na kwa eneo la Kerege zoezi ni ukarabati wa bomba la zege la nchi 54 kazi ambayo inaendelea na itamalizika ndani ya wiki hii," alieleza Mhandisi Mkindi.

Pia Mhandisi Mkindi alisisitiza kuwa pamoja na maboresho haya makubwa, huduma ya majisafi kwa wakazi wa Mapinga inaendelea kupatikana kupitia matoleo ya bomba kubwa la inchi 72, hakuna maeneo yanayokosa huduma ya maji.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Mapinga, Benjamin Nko, alisema ni faraja kwa wananchi kuona DAWASA wanatatua changamoto ya maji yasiyolipiwa ambayo huwa ni sababu mojawapo wananchi kukosa maji ya uhakika.

"Naishukuru serikali kupitia DAWASA kwa ujumla kwa jitihada hizi za kutatua tatizo la maji yasiyolipiwa tuna imani na ujio wa marekebisho haya kwa kuwa yataleta manufaa makubwa katika mtaa wetu," alisema Nko.

Miongoni mwa vipaumbele vya (DAWASA) ni udhibiti wa kiasi cha maji yasiyolipiwa na kuhakikisha huduma ya majisafi inawafikia wananchi wote.



Mafundi wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira (DAWASA), wakiendelea na matengenezo ya bomba la inchi 8, katika kata ya Kiluvya mkoani Dar es Salaam jana, kwa lengo la kuongeza msukumo wa maji katika maeneo ya Kiluvya kwa Sumaye, Makurunge, Kwa Omary, Tondori na Manzense. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mbunge awajengea soko wajasiriamali

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MBUNGE wa Jimbo la Masasi, Geofrey Mwambe, hatimaye amemaliza kilio cha wananchi wa Kata ya Chanika Nguo cha kuomba kujengewa soko la kisasa la wajasiriamali wa kata hiyo kwa kuwapatia msaada wa Sh. milioni 7.5 ili kuanza ujenzi huo.

Aidha, ameahidi kufanya kila juhudi za kuhakikisha anawaleta wawekezaji mbalimbali watakaokuja kuanzisha viwanda vidogo ndani ya Jimbo la Masasi lengo likiwa ni kupunguza changamoto ya ajira kwa vijana na kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja katika jimbo hilo.

Aliyasema hayo jana wakati alipokuwa akizungumza na wananchi wa kata ya Chanika Nguo alifanya ziara ya kusikiliza na kupokea kero za wananchi wa kata hiyo.

Alisema kuwa Masasi ni kitovu cha biashara kwa ukanda wa mikoa ya kusini, lazima kuwe na mikakati thabiti ya kuwafanya wananchi wanakuwa wafanyabiashara wakubwa.

Alisema njia pekee ya kuwanyanyua wajasiriamali ni kuwajengea masoko ya kisasa yatakayowakutanisha pamoja na kuendesha shughuli zao kwa utulivu.

"Leo nawapatia hizi Sh. milioni 7.5 ili mjenge soko la kisasa na kama zitakuwa zimekwisha kabla ya soko kukamilika basi nitawaongezea dhumuni langu ni kuona wajasiriamali wote mnafanya kazi pamoja na mitaji yenu inakuwa," alisema Mwambe.

Mwambe alisema ameshajenga soko la wajasiriamali katika kata za Mumbaka na Malika na sasa wajasiriamali wa maeneo yao wameshaanza kufanya shughuli zao na atahakikisha kila kata anajenga soko kwa ajili ya wajasiriamali, jimbo hilo lina jumla ya kata 14. Wakizungumza baada ya kupokea hundi hiyo ya Sh. milioni 7.5, wananchi hao akiwamo Jafari Msusa, mkazi wa Kata ya Chanika Nguo, alisema wanampongeza mbunge huyo kwa kuwapatia fedha hizo kwa kuwa sasa wana matumaini ya kufanya shughuli za pamoja na kwa utulivu.

Naye Saidi Afidhi, mkazi wa kata hiyo alisema, wananchi wa kata hiyo wanajitolea kwa hali na mali kuchangia nguvu kazi katika ujenzi wa soko kwa kuwa kilichofanywa na mbunge.

Akiwa katika kata hiyo, Mwambe alipokea kero mbalimbali kutoka kwa wananchi ikiwamo kero ya upatikanaji wa huduma ya maji, umeme, miundombinu ya barabara na ameahidi kuzipatia ufumbuzi wa kudumu.

# Mpango: wajasiriamali waruhusiwe kufundisha

**Na Renatha Msungu,**
MBEYA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amemtaka Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Triphonia Kisiga, kuwaruhusu wajasiriamali kwenda vyuoni kutoa elimu ya ujasiriamali kwa vijana ya namna walivyopata mitaji, walivyoanza ujasiriamali.

Lengo ni kuhamasisha kundi hilo kujiunga na ujasiriamali badala ya kusubiri kuajiriwa.

Dk. Mpango alisema hayo jana wakati akitembelea mabanda mbalimbali kwenye maonyesho ya wakulima Nanenane yanayofanyika kitaifa jijini hapo.

Alisema wajasiriamali wanafanya mambo makubwa kwenye sekta ya kilimo, ni vyema jiji na baadhi ya wajasiriamali wa chini wakaweka utaratibu wa kuwaruhusu kwenda kuwafundisha kundi hilo.

"Kuna vijana wengi wanafikiria kuajiriwa peke yake, lakini kumbe kwenye ujasiriamali kuna ajira hivyo ni vyema wakaenda kuwafundisha," alisema Dk. Mpango.

Aliwapongeza wafugaji katika banda la ufugaji ndege mbalimbali wakiwamo kuku na bata kwa uwekezaji wa mifugo waliofanya unaowasaidia kuwainua kiuchumi na familia zao.

Alisema ujasiriamali kama huo unapaswa kufanywa na vijana wanao hitimu vyuo, ili wapige hatua kiuchumi na kujiajiri.

Naye Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema serikali imeonyesha utayari wa kuwekeza kwenye sekta ya kilimo na kwamba wakulima hawawezi kukua bila kuheshimu sekta hiyo.

Alisema bila kuwekeza kwenye sekta ya fedha wasingefika walipo na kuzipongeza benki za NMB na CRDB kwa kutoa mikopo ya riba nafuu kwa makundi mbalimbali.

"Benki ambazo hazitaelewa hili la mikopo ya riba nafuu hatutafanya nazo kazi," alisema Bashe.

Alisema baada ya maonyesho hayo Makamu wa Rais atashuhudia utiaji saini wa miradi ya Sh. bilioni 400 ya umwagiliaji ikiwamo kuzindua skimu za utoaji ruzuku za mbolea.

Kwa upande wake, Meneja Kanda ya Mbeya wa Benki ya NMB, Staraton Chilongola, alisema kwa miaka mitano wametoa mikopo ya Sh. trilioni 1.2 kwenye sekta ya kilimo kwenye mazao ya kipaumbele.



Waziri wa Mifugo, Mashimba Ndaki, akikagua moja ya bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda mkoani Katavi, alipotembelea banda la maonyesho ya wakulima Nanenane, katika viwanja vya John Mwakangale, jijini Mbeya jana, (kulia) ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Jamila Yusuph Kimaro. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wizara yatakiwa ufumbuzi w'biashara kuhamia nchi za nje

**Na Ibrahim Yassin,** MBEYA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ameitaka Wizara ya Viwanda na Biashara kutafuta ufumbuzi wa wafanyabiashara wa nchini kuhamia Zambia na Malawi.

Dk. Mpango aliyasema hayo jana jijini hapo alipotembela mabanda ya maonyesho ya 19 ya wakulima yanayoendelea uwanja wa John Mwakangale, jijini hapo, huku akitaka kuweka mazingira rafiki kuondoa tatizo hilo.

Alisema katika ziara zake na za Waziri Mkuu, malalamiko yaliyoko kwenye mipaka ni kandamizi yanayosababisha wafanyabiashara kuhamia nchi jirani ikiwamo Zambia na Malawi hali inayoikosesha nchi mapato.

"Naagiza Wizara ya Viwanda na Biashara na wizara zingine kaeni mlione hili kwa jicho la ziada na mtafute ufumbuzi sababu ya wafanyabiashara kuhamia nchi jirani na nipate majibu kwa muda mfupi," alisema Dk. Mpango.

Alisema kufuatia changamoto za kilimo zilizowakumba wakulima ikiwamo za pembejeo, ilitokana na uwapo wa vita vya Ukraine na Russia pamoja janga la UVIKO-19, serikali imetenga Sh. bilioni 551 ikiwa ni bajeti kubwa ikilinganishwa na mwaka 2020/21 Sh. bilioni 224.

**Alisema katika ziara zake na za Waziri Mkuu, malalamiko yaliyoko kwenye mipaka ni kandamizi yanayosababisha wafanyabiashara kuhamia nchi jirani ikiwamo Zambia na Malawi hali inayoikosesha nchi mapato.**

# Wakulima watakiwa kujifunza kwenye Nanenane

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

WAKULIMA nchini wameshauriwa kufika kwenye maonyesho ya kilimo Nanenane Kanda ya Mashariki ili kujifunza mengi ikiwamo afya ya udongo na matumizi ya mbolea kuboresha kilimo na kuepukana na kupata mavuno machache.

Naibu Mkurugenzi wa Utafiti wa Kilimo Kanda ya Mashariki (ARI), Dk. Catherine Senkoro, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kikao cha watafiti kutoka kanda zote za kilimo ARI Tanzania waliokutana kufanya maandalizi ya maonyesho ya wakulima Kanda ya Mashariki, mwaka huu.

Dk. Senkoro ambaye ni Mkuu wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo ARI-Mlingano - Tanga, alisema wakulima watanufaika na elimu ya afya ya udongo, kutokana na elimu hiyo kwenye maonyesho hayo.

Aidha, alisema kituo hicho hufanya utafiti na kuhakikisha wakulima wanafahamu afya ya udongo na teknolojia na matumizi ya mbolea za asili na viwandani katika kuleta tija kwa mkulima.

"Huwa tunafanya tathmini na kuhakikisha kabla mkulima hajaingia shambani, ajue atalima mazao gani kwenye udongo huo na atatumia mbolea za aina gani za mchanganyiko za viwandani na asili au laa, yote hiyo ni kuongeza rutuba ya udongo na kuleta tija kwenye kilimo," alisema Dk. Senkoro.


Alisema lengo la kutoa elimu hiyo kwa wakulima ni kuhakikisha wanapata teknolojia ambazo zitaboresha uzalishaji wa mazao na kuleta tija kwenye kilimo kwa mkulima na taifa kwa ujumla.

Naye Mtafiti Kiongozi kitaifa katika tathmini ya rasilimali ardhi, ARI- Mlingano, Dk. Sibawei Mwangwa, aliwashauri maofisa ugani kutoa elimu ya udongo kwa kutumia ramani za udongo ili kuwafanya wakulima kunufaika na kilimo.

Dk. Mwangwa alisema, elimu hiyo kwa wakulima itawafanya kutambua kuwa hawawezi kuwekeza sehemu bila kuona tathmini ya udongo, maji na mbolea.

Aliwashauri wakulima hao kutembelea banda la maonyesho ya utafiti wa kilimo ARI lililoko kwenye viwanja hivyo ili kujifunza mambo mengi zaidi yaliyoko.

Naye mtafiti wa mazao yanayostahimili ukame kutoka Kituo cha Utafiti ARI - Ilonga - Morogoro, Salvatory Kundi, aliwashauri wakulima kuzingatia na kutumia ushauri unaotolewa na watafiti wa kilimo ili kupata mazao bora na kuleta tija kwao na taifa.




Ukurasa 12

## Mbinu chafu zaanikwa, Ruto ashiriki mdahalo, Raila aingia mitini



Ukurasa 14

Ni hali inayoonyesha ugumu demokrasia kutamalaki



Ukurasa 14

SURA 4 ZA MSTAAFU DK. BILAL

## Afunguka fumbo aliloamua kisiasa, ukazuka mjadala uliobaki kitendawili


# siasa

JUMATANO AGOSTI 3, 2022

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe


RAIS NA POLISI MPYA

# Kamati itaje mbinu kukabili uhalifu wa kisasa, ugaidi, uasi

• Konda, dereva wakiajiriwa mlungula kupungua barabarani

**Na Gaudensia Mngumi**

RAIS Samia ameunda kamati na sekretarieti kwa lengo la kumshauri njia bora ya kuunda na kufikia mabadiliko ya utendaji kazi wenye matokeo bora kwenye vyombo vinavyoshughulikia haki jinai au 'crimal justice.' Ni taasisi kama majeshi ya polisi , mahakama, magereza,upelelezi wa jinai na uendeshaji wa mashtaka.

Mambo yanayoanza kufanyiwa kazi ni pamoja na kuchunguza na kuboresha Jeshi la Polisi ili kuwa na jeshi imara la kuwatumikia Watanzania.

Wakati kamati inayoongozwa na Jaji Mkuu mstaafu Othman Chande, inaanza kazi ya kuchunguza na kutoa mapendekezo ya kuwa na polisi bora ,chombo hicho kinakabiliwa na changamoto nyingi na wakati mwingine mpya na za kutisha.

Mathalani, mitandao ya kisasa tena iliyosukwa ya kihalifu inayotumia teknolojia na silaha za kisasa ikiwamo ya madawa ya kulevya na ugaidi.

Aidha, kuna uhalifu mwingine unaweza kufananishwa na uhalifu wa viwango vya juu ambao wakati mwingine unashambulia polisi vituoni, mfano matukio yaliyowaua polisi na kuwapora silaha kwenye vituo vya Ikwiriri, Kimanzichana na Stakishari.

Lakini pia, mashambulizi ya mauaji ya raia na viongozi yaliyoripotiwa Kibiti mkoani Pwani pamoja na mtandao wa kihalifu ya kiuasi kama mashambulizi yanayotokea kwenye mpaka wa kaskazini wa Msumbiji, ambayo nayo yanatishia amani mikoa jirani kama Ruvuma.

Kwa ujumla kulisuka na kuliunda upya jeshi la polisi kunahitaji kutizama 'maendeleo na usasa' kwenye uhalifu kuanzia ugaidi, uasi, biashara ya kusafirisha binadamu na mitandao ya dawa za kulevya na silaha.

Changamoto nyingine inayowakabili polisi leo ni kuhakikisha ulinzi wa haki za binadamu na jinsi gani wanawajibika wenyewe ndani ya jeshi lao ili wasiwe chanzo cha lawama wakati wakitekeleza majukumu yao.

Eneo hili linahitaji kufikiriwa na kuchunguzwa zaidi kwa vile wakati mwingine polisi hawaheshimiwi na raia kwa vile wanaonekana kuwa sehemu ya changamoto za kijamii.

Mathalani, kuwapo kwa tuhuma za raia kuuawa wakiwa chini ya polisi, kwa kurejea tukio la maofisa kadhaa wa polisi wanaoshitakiwa mkoani Mtwara kwa mashtaka ya mauaji ya kijana mfanyabiashara Mussa Hamisi mkazi wa Nachingwea.

Kijana huyo anadaiwa kuuliwa na mwili wake kutupwa .Licha ya kesi kuwa mahakamaani ni hoja iliyoibua maswali kuwa polisi wanawezaje kutuhumiwa na kujichunguza wenyewe?

Hivyo ni vyema kuangalia namna bora ya kuwa na chombo cha kuwachunguza na kuwawajibisha polisi iwapo kutakuwa na tuhuma ili kuondokana na mazingira yanayoweza kukwamisha sheria kuwaadhibu na haki kutendeka.

Polisi wanapokuwa kwenye majukumu yao kuna madai ya kuwabambikia raia kesi na kusababisha usumbufu mkubwa kwa watuhumiwa na jamaa zao, hili nalo ni la kuzingatiwa.

**KUPUUZA SHERIA**

Kamati inapofanyia kazi suala la raia kuvunja sheria kwa makusudi na kuzipuuza linazidi kutia fora.



Mtuhumiwa akiwa chini ya ulinzi. Suala la kusimamia haki ya wanaofanya jinai ni moja ya kazi za Polisi. **PICHA: MTANDAO**

Polisi wana changamoto kubwa ya kuwaaminisha na kuwawezesha watu kutii sheria bila shuruti kwa vile wengi hawathamini wala kujali sheria.

Kwa mfano, madereva wa bodaboda wanafanya watakavyo barabarani. Kwenye jamii kuna kuua watu, mikasa ya kufukua makaburi na kuchukua viungo vya wafu. Wenza kuuawa kwenye ndoa, watu kutunza na kuingiza wahalifu na silaha nyumbani kwao . Aidha, kusafirisha na kuhifadhi wahamiaji haramu yote ni mambo yanayoonyesha kuwa kuna kuvunja sheria bila hofu.

Wapo baadhi ya watu wanaounda mitandao ya kihalifu kuiba na kusumbua raia wakiwamo vijana kama panya road na hata wengine wanaoangusha magari barabarani ili kupora.

Jambo jingine ni kuchoma watuhumiwa kama vibaka kwa kisingizio cha hasira kali. Wapo wengine wanaosingiziwa na kuuliwa bila huruma kwa madai ya wizi.

Kuna imani za kishirikina za kusingizia watu uchawi na kuwaua , wapo wachache wanaamini kuwa wananyonywa damu na kuwaua mumiani. Yote hayo ni changamoto kwa polisi wanaofanyakazi na raia mbumbumbu.

Ikumbukwe wakati mwingine mifumo ya haki jinai (criminal justice systems) ambayo huanzishwa na jamii au serikali ili kuzuia na kudhibiti uhalifu na ghasia ili kulinda na kuendeleza haki za msingi zinawataka polisi kuzingatia haki.

Hivi polisi wanaweza kufanyakazi bila ubabe katika mazingira magumu ya watu wanaokataa kutii sheria kama hayo?

Kuna madai kuwa polisi wa Afrika ni wababe maana walirithi ubabe kutoka kwa polisi za mkoloni hivyo kubakia na sifa za kukandamiza na kutokujali watuhumiwa na kuwafanya waogope zaidi na kuwanyenyekea.

Kuna maelezo kuwa wakati mwingine ukiwa rumande unaweza kukabiliwa na vitisho mfano hata kukatazwa kufukuza mbu wanaokung'ata kwa maelekezo kuwa hawana shamba, kuna haja ya kuangalia na kurekebisha hali hiyo ya kuwafanya watuhumiwa kuwa duni na hata kushindwa kujitetea kisa tu wako rumande, lakini pia kufanya kampeni ya kitaifa kila mara kuhakikisha ufahamu na utii wa sheria.

INAENDELEA UK. 12

VIMBWANGA UCHAGUZI KENYA

# Mbinu chafu zaanikwa, Naibu Ruto ashiriki mdahalo, Raila aingia mitini

**Na Mwandishi Wetu**

MISHALE ya saa inapokaribia Agosti 9 ili Wakenya wapige kura kwenye uchaguzi mkuu, mikasa mbalimbali imeibuka hivi karibuni ikiwamo Muungano wa Naibu Rais kutuhumiwa kununua kadi za wapigakura.

Aidha, kuna tuhuma za kujaribu kuwahonga mawakala wa vyama na kuwapanga machifu kushawishi watu kupigia upande fulani ni masuala yanayotikisa uchaguzi zikiwa zimesalia takriban siku sita.


Muungano wa Kenya Kwanza wa Naibu Rais, William Ruto na Muungano wa Azimio la Umoja One wa Kenya chini ya Raila Odinga mwishoni mwa wiki walizusha dhoruba wakishutumiana kwa kujihusisha na mbinu chafu ili kushinda kinyang'anyiro hicho kilichokuwa na mashabiki wengi.

Daktari Ruto amemshukia Rais Uhuru Kenyatta kwa kuwashurutisha machifu na watumishi wengine wa umma kutumia nyadhifa zao kumsaidia Odinga kushinda kiti hicho cha urais kinachodaiwa ni cha kurithishwa.

Ununuzi wa mawakala wa Azimio, kama Chama cha Jubilee, kupitia Katibu Mkuu, Jeremiah Kioni, kilidai kuwa Ruto pia alikuwa na njama ya kuwanunua mawakala wa Azimio, hasa eneo la Mlima Kenya, ambako anaungwa mkono na umati wa wapigakura.

Wakati huo huo, Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya Majimbo (IEBC) imekiri kuwapo visa vya watu wasio waaminifu kuzunguka nchi nzima kununua vitambulisho kutoka kwa waliojiandikisha kupigakura kabla ya uchaguzi.

“Zimetufikia taarifa kwamba kuna baadhi ya watu wanaozunguka katika maeneo ya watu wakinunua vitambulisho kutoka kwa wapigakura,” Mwenyekiti wa IEBC,” Wafula Chebukati anasema wiki iliyopita.



Ruto (kushoto) na Odinga waliokuwa washiriki mdahalo wa wagombea urais, lakini Odinga akasusia. **PICHA: MTANDAO**

> “Mjadala ulikuwa kama mazungumzo. Kutokuwapo kwa Raila ilikuwa bahati mbaya.

Hata hivyo, hakuna ushahidi wa madai ya kununua vitambulisho Katibu Mkuu wa Democratic Action Party of Kenya (DAP-K) Eseli Simiyu, naye anaishutumu Kenya Kwanza ya Ruto kuwa inajihusisha na ununuzi haramu wa vitambulisho katika eneo la Magharibi, lakini hakuweza kuthibitisha.

**KUSUSA MDAHALO**

Wakati uchaguzi ukiingia dakika za mwisho bado Wakenya wana kumbukumbu za Raila Odinga, kususia mdahalo wa wagombea urais wiki iliyopita.

Timu yake ya kampeni ilisema anasusia huku ikimtuhumu mpinzani wake kwa kujaribu kukwepa mada za ufisadi.

Odinga (77) na Naibu Rais William Ruto ( 55) hawakukutana kwenye ulingo wa madai kuwa mdahalo ambao mpinzani wake anaelekeza ni aina gani ya maswali ya kumuuliza, Raila asingeushiriki. Raila alijibiwa, Ruto akimkejeli kwa uamuzi huo, ni kutokana na kukwepa aibu.

Ruto alimchombeza Raila akisema: “Njoo unikabili kwenye mdahalo hata kama huna mpango na Wakenya.”

Hata aliposusa, Ruto alisimama peke yake kwenye mdahalo Jumanne Julai 26, baada ya mpinzani Raila Odinga kuususia na mgombea mwingine, George Wajackoyah, pia kutoshiriki, akimuacha mshindani mwingine - David Mwau, kujibu maswali peke yake.

Licha ya hayo, Ruto alijibu maswali kwa dakika 90, akimshutumu Odinga kukaa pembeni kwa kuhofia kujibu maswali magumu. “Mpinzani wangu hayupo hapa kwa sababu hana mpango, hana ajenda,” Ruto anadai.

Anapoulizwa kuhusu madai ya ufisadi na kiu ya kumiliki mali, hasa ardhi, Ruto alipuuza akisema: “Kipande chochote cha ardhi nilicho nacho nimekipata kihalali.” Akaongeza: “Vita dhidi ya ufisadi vimefanywa kisiasa na mimi ndiye mwathiriwa mkuu. Inatosha sasa”.

**RAILA HOLA**

Brian Wanyama, mchambuzi wa masuala ya kisiasa, anasema Raila alikosa fursa ya kueleza masuala yake kwa ufasaha kwa wapigakura wakati wa mjadala huo, ambao anasema uligeuka kuwa kipindi cha maswali na majibu. Mjadala ulikuwa kama mazungumzo. Kutokuwapo kwa Raila ilikuwa bahati mbaya, anaongeza.

Pia anaelezea kuwa Ruto hakuonyesha ufanisi, akimpa alama za chini ya wastani kwa sababu alikosa mpinzani wa hakueleza wazi mpango wake wa kiuchumi jinsi ilivyotarajiwa.

“Mjadala ulikuwa kama mazungumzo. Kutokuwapo kwa Raila ilikuwa bahati mbaya,” Wanyama anaiambia mtandao wa The Africa Report.

**ODINGA KUATHIRIKA**

Wachunguzi wa mambo wanaona kuwa Odinga kukwepa mdahalo wa urais kumesababisha kutopinga madai dhidi yake kutoka kwa Ruto, hivyo kumpa nafasi ya kuibuka kidedea dhidi yake.

**MITANDAO**

## Kamati itaje mbinu kukabili uhalifu wa kisasa, ugaidi, uasi

**INATOKA UK. 11**

**KUWAPO RASILIMALI**

Suala la uhaba wa rasilimali na nyenzo muhimu za kushughulikia uhalifu na kuuzuia ni muhimu ili kuwe na haki, kazi zifanyike kwa ufanisi na polisi wadumishe utulivu na amani ya umma ni lazima wawe na mafunzo yanayozidi wahalifu wa ‘kisasa’, mishahara ya kuridhisha, makazi bora na vitendea kazi vikiwamo vya kutosha na vya kisasa vinavyozidi vya mitandao na magenge ya wahalifu.

Wawe na magari ya kisasa barabarani, mitandao ya mawasiliano, boti , helikopta na fedha za kusafirisha watuhumiwa, kufanya uchunguzi na kuachana na madai kuwa hakuna fedha za kusafirisha watuhumiwa kutoka vijijini kwenda vituo vya polisi.

**MICHAKATO AJIRA**

Vikwazo vingine vya kushughulikiwa ni pamoja na michakato yenye kasoro ya kuajiriwa kwa sababu ya madai ya ajira kuhusishwa na kufahamiana au upendeleo, hivyo kuwe na vigezo na utekelezaji wake ufuatiliwe mara kwa mara baada na kabla ya ajira.

Ndiyo maana wakati Rais Samia anawaapisha viongozi wapya wa jeshi hilo akiwamo Inspekta Jenerali Camillus Wambura, alisema ‘tukichunguza tutakutana na vyeti feki vingi” lakini pia akigusia vituko vinavyotokea barabarani.

**YANAYOJIRI BARABARANI**

Suala la madereva na polisi wa usalama barabarani kuvunja sheria ni jambo linalochafua polisi wakituhumiwa kuwa wanafanya ndivyo sivyo.

Tume inapoangalia namna ya kuboresha jeshi hilo kwa tija, hoja ya adha barabarani itahitaji jicho la kipekee. Ni kwa sababu watu wanaowapa polisi ‘vijisenti’ hawaoni kuwa ni kuvunja sheria, wakichukulia kama namna bora ya kufanikisha kazi zao.

Ni kwasababu wanachukuliwa kuwa wanatoa Shilingi 1, 000 au 2,000 ambazo kwao si nyingi. Madereva wa daladala kwa mfano wanaokusanya takribani Shilingi 200,000 kila siku kutoa 1, 000, hakuwaumizi.

Wanaona kuwa ni fedha kidogo wala haiathiri uchumi wao, lakini wangekuwa wanatoa kwenye mishahara yao ya 500,000 kwa mwezi wasifanya makosa ili kulinda mapato yao.

Aidha, wanaopokea fedha hiyo wanaiona kuwa ni nyingi kutokana na idadi yake kwa siku mfano wakipata madereva 20 wanaotoa kati ta Shilingi 1, 000 hadi 3,000 kila siku ni fedha nyingi zinapoingia kwenye mfuko wa mtu mmoja.

Ni kipato kikubwa ambacho hakilipiwi kodi wala hakina tozo na wala hakinufaishi taifa.

Madereva wanatakiwa kupata mafunzo ya uchumi kuwa iwapo watatoa wastani wa Shilingi 100,000 kila mwezi kwa wasimamizi wa usalama barabarani athari yake ni ipi kiuchumi?

Maderava hasa wa daladala hawana uchungu kwa vile fedha wanazotoa hazilipiwi kodi. Pengine ni wakati wakufikiria jinsia ya kuwaingiza kwenye mifumo rasimi ya kodi ili kulipa kodi ya mshahara ya PAYE kila mwezi. Aidha, kuwapa mikataba ya ajira na kutungwa sheria ya kukataza na kuharamisha mazoea hayo lakini pia kuwa na utaratibu bora na wa kielektroniki wa ukaguzi wa magari na utozaji faini kwa madereva.

Madereva hao wanachohakikisha ni kulipa fedha za mwenye basi kila siku na kiasi chote kingine wanachopata ni chao, hakitozwi kodi wala hakuna wa kuwafuatilia, hivyo hutumia udhaifu huo kuwaingiza wasimamizi wa sheria barabarani kwenye mtego wa kuwapa chochote ili kuficha makosa yao.

Ni wakati wa kuwafundisha pia athari za kutoa fedha hizo kwenye uchumi na maendeleo ya taifa. Kuna faida gani kutoa kila mwezi 50,000 ili kuendesha gari lenye hitilafu? Je kwa upande wa uadilifu wa utendaji kazi wa jeshi ni kwa namna gani kutoa mlungula kunaathiri ufanisi wa huduma za usafiri na maadili ya kazi?

UCHUNGU UCHAGUZI CCM

# Ni hali inayoonyesha ugumu demokrasia, haki kutamalaki

## • Makovu, hofu za mwaka 2020 vinavyoibuka upya

**Na Sabato Kasika**

MWEZI mpya Agosti unapoanza, CCM inaendelea na uchaguzi wa ndani ngazi ya kata, huku kuchagua viongozi kwenye mashina na matawi kukigubikwa na figisu na vituko vingi hata maeneo mengine ukifutwa.

Mathalani, wagombea kunyimwa fomu kwenye baadhi ya maeneo, viongozi kuteuliwa badala ya kuchaguliwa na wanachama ni hali iliyosababisha baadhi ya makada kutishia kurudisha kadi za uanachama na kukifanya chama kufuta uchaguzi kwenye kata ya Mahina iliyoko wilayani Nyamagana mkoani Mwanza.

Kata ya Mahina umeripotiwa kuwa moto mkali kwenye uchaguzi huo, baada ya malalamiko mengi kuibuliwa kama viongozi kuteuliwa badala ya kuchaguliwa katika mashina 80 na matawi manane.

Wakati kukiwa na changamoto hiyo kwenye baadhi ya maeneo nchini, Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Abdulrahman Kina, anawahimiza makada hasa wanawake na vijana kujitokeza na kuchukua fomu kuwania uongozi wa ndani ya chama hicho.

Katika wito wake huo kwa makundi hayo kuchukua fomu, anawapa matumaini kuwa haki itatendeka na kwamba hakuna wa kumtisha mwenzake.

Kufuatia kauli ya kiongozi huyo wa juu ndani ya chama hicho tawala, Nipashe inazungumza na baadhi ya wachambuzi na wadau wa siasa, kupata maoni yao jinsi wanavyouchukulia na kuutazama uchguzi huo.



Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Abdulrahman Omar Kinana (wa kwanza kushoto), akikutana na wana CCM. **PICHA: MTANDAO.**

### UCHAGUZI SI LELEMAMA

Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Lilian Liundi, anasema kauli hiyo ya Kinana ni kutaka kuwaandaa kisaikolojia vijana ili watambue kuwa kuwania uongozi si lelemama.

Anasema, lingine ni kwamba, Makamu Mwenyekiti anatekeleza kile ambacho kipo katika sera za chama hicho na pia kwenye mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo serikali ya CCM imesaini ikiwamo suala la usawa wa kijinsia katika uongozi la kuwa na uwiano wa wanawake na wanaume viongozi kwa utaratibu wa 50/50.

"Kuwania uongozi si utani kwani unakuta nafasi ina mtu, hivyo kumwondoa kirahisi haiwezekani, kwani naye anafanya mbinu za kubaki madarakani, ndiyo maana Kinana ametoa kauli hiyo ambayo ninaamini ina lengo la kuwaandaa kisaikolojia kupambana," anasema Lilian.

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP anaongeza kuwa katika kuwania uongozi, watu wanashindana kwa hoja, na kwamba ni vyema wanaochukua fomu watambue hilo na kuachana na fikra za kutotendewa haki.

"Nimpongeze Kinana kwa kauli yake ya kuhimiza wanawake kujitokeza kuwania uongozi, hilo ndilo ambalo tumekuwa tukilihimiza katika vyama vya siasa, ili kuleta usawa wa kijinsia kwenye uongozi," anasema.

> “ Niwaombe kinamama mkachukue fomu za kuwania nafasi za uongozi CCM, msiogope nendeni mkachue fomu mpambane na wanaume. Pia nataka niwasihi vijana gombeeni hizo nafasi.

### KURUDISHA HAKI

Mchambuzi wa masuala ya siasa Said Msonga, anasema anachokifanya Kinana ni kurudisha makada kwenye mstari baada ya wengine kuanza kukata tamaa kutokana na uchaguzi uliopita.

Anafafanua kuwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, baadhi ya makada walioshinda kura za maoni, majina yao yakakatwa na kuwekwa waliokuwa na kura chache.

Aidha, hali hiyo iliwakatisha tamaa, hivyo uzoefu wa chama katika uchaguzi uliopita, uliwafanya baadhi ya makada kudhani kwamba hata wakiwania uongozi, wachache ndiyo watakaoamua nani ashinde.

Mchambuzi huyo anasema, Kinana anaanza kuondoa dhana hiyo vichwani mwa wanachama kwamba haipo tena badala yake mgombea atapatikana kwa haki kulingana idadi ya kura alizopata na si vinginevyo.

"Komredi Kinana anakijua chama ndani na nje, anaamini kwamba, yaliyojitokeza miaka ya nyuma yameacha baadhi ya makada wanawake na wanaume kukosa mwamko wa kushiriki uchaguzi," anasema.

### NI SAWA, LAKINI

Wakili Anna Henga ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), ambaye anasema hadi aone wanawake wanapewa uongozi kwa wingi ndipo ataiamini kauli hiyo.

Henga anasema, mara nyingi kauli za wanasiasa zimekuwa zikiishia majukwaani bila kuwa na mipango ya kuwafanya wanawake na makundi maalum kushika nafasi mbalimbali za uongozi.

"Ni jambo la kufurahia kama kweli wana nia ya dhati ya kuingiza masuala ya jinsia. Ila mara nyingi wamekuwa wakisema hivyo, lakini hakuna mipango ya kuhakikisha idadi ya wanawake na wanaume inakuwa sawa katika uongozi, lakini ngoja tusubiri tuone," anasema Henga.

Anataka mwanachama asichaguliwe kwa jinsi yake, bali kwa uwezo wa kuongoza na kwamba, wanawake wenye uwezo wa kuongoza ni wengi ila wanaogopa vitisho katika vyama vyao na kusita kujitokeza.

"Kauli ya Kinana kuwa haki itatendeka hakuna wa kumtisha mwenzake, ni wazi kwamba wanawake wamekuwa wakitishwa, lakini kwa sababu wameondolewa hofu, basi wajitokeze kwa wingi, ingawa binafsi niansubiri kuona haki ikitendeka katika uchaguzi huo," anasema.

### MAELEKEZO YA KINANA

Makamu Mwenyekiti Bara amefanya ziara katika mikoa ya Katavi, Rukwa, Songwe na Mbeya, akiwa Rukwa, anatoa maelekezo kwamba, hakuna masultani wa kukaa madarakani milele na kuhimiza wanawake na vijana kuchukua fomu kuwania uongozi.

"Niwaombe kinamama mkachukue fomu za kuwania nafasi za uongozi CCM, msiogope nendeni mkachue fomu mpambane na wanaume. Pia nataka niwasihi vijana gombeeni hizo nafasi," anasema Kinana.

Anasema uchaguzi ukifika, nafasi zitakuwa wazi na kila mtu ana haki sawa na mwenzake na kwamba hakuna masultani wa kukaa madarakani milele, na kufafanua kuwa chama kina uchaguzi kila baada ya miaka mitano.

"Wanaowachagua wanaCCM, ni wanachama wakikupenda, wakikuheshimu na wakithamini mchango wako watakupa kura lakini wasipokuthamini watakunyima. Nafikiri na ninyi mnawafahamu wajumbe sio watu wazuri," anasema.

Anasema wajumbe wanaweza kumwambia mgombea kuwa asihofu watampa kura, kisha wakamtosa, lakini akawataka wanawake na vijana wagombee, watashinda, akisisitiza kuwa haki itatendeka hakutakuwa na upendeleo.

JUKWAA LA VIONGOZI

SURA 4 ZA MSTAAFU DK. BILAL

# Afunguka fumbo aliloamua kisiasa, ukazuka mjadala uliobaki kitendawili

- Kitaaluma darasani amebobea Fizikia ya mabomu
- Katibu Mkuu 'kiboko' ya waandamanaji vyuo vikuu

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR



Makamu wa Rais wa awamu ya nne , Dk. Bilal akiwa kwenye majukwaa ya kisiasa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

LEO hii mtu anapogeuza sura kumkumbuka na kumuangalia Makamu wa Rais Mstaafu Dk. Mohammed Gharib Bilal, wengi wanamtenga katika sifa ya ya uanasiasa, tena katika ngazi ya juu.

Hiyo ni sifa ya mwisho, huku kukiwepo nyingine nyingi, ikianza na kuwa mwanasayansi aliyebobea, wakati fulani akiwa mtaalamu bingwa pekee wa fizikia ya mabomu nchini.

Ndani ya wajihi huo wa kisanyansi, mwaka 1988 anabaki katika alama kuchangia kampeni ya kuinua sayansi Zanzibar, hali kadhalika, ameshiriki kuasisi na kuendesha taasisi ya kisayansi,COSTECH.

Sifa yake nyingine ni mwanazuoni; Dk, Bilal baada ya kuhitimu masomo mwaka 1976 akikwaa kishangilio kinachotangulia jina, Daktari, alianza kufundisha katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Idara ya Fizikia ya Nyuklia, ambako baadaye aliteuliwa kuiongoza.

Hata hivyo, kazi hiyo ya kufundisha katika vyuo vikuu, msomi huyo ambaye ana wajihi wa upole na mwenye msimamo katika anachoamua, alianza akiwa nchini Marekani, baada ya kuhitimu masomo yake ya uzamili.

Pia, mwaka 1983 akiwa nchini akashiriki kuunda chombo cha kitaasisi kinachosimamia rada nchini na hatimaye mwaka 1988 akiwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, aliteuliwa kuongoza Kitivo cha Sayansi chuoni hapo.

Ni mwaka huo 1988, anabaki katika alama ya kuchangia kampeni ya kuinua sayansi Zanzibar, hata baadaye ukawa mradi rasmi na mkubwa katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Sura ya tatu, ni pale mwaka 1990 Dk. Bilal alibadilishiwa majukumu kuwa mtendaji mwandamizi, kwa maana ya Katibu Mkuu wa wizara mpya ya; Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, akiongozwa na Waziri Benjamin Mkapa, alikotumikia hadi mwaka 1995.

Ni zama anazokumbukwa kuwa 'injini' ya mageuzi nchini katika elimu, hata alivyokabiliana na maandamano ya wanafunzi waliopinga kuchangia gharama, hasa vijana wake wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, walioweka kambi ofisini kwake wakishinikiza ifutwe, huku wakipambana na msimamo mkali wa Katibu Mkuu huyo, aliyefahamika fika kwa wasomi hao shuleni.

Pia, katika wadhifa huo, ndiye alifanya kazi ya uasisi wa Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT) ambacho sasa kinakwea na nyenzo muhimu katika elimu ya taifa .

### SAFARI ALIKOTOKA

Kimsingi, mzaliwa huyo wa Februari 6, mwaka 1945 mjini Unguja, amesoma katika Shule ya Msingi Makunduchi, alikomaliza elimu ya msingi na akaendelea na Sekondari ya Beit-el-Ras hadi mwaka 1962 alipohitimu.

Baada ya hapo, akafaulu na kuendelea na kidato cha tano katika Shule ya Sekondari Lumumba mjini Unguja. Hapo umahiri wake darasani ukampatia 'ofa' kwenda katika Chuo Kikuu, Howard Washington, Marekani alikohitimu mwaka 1967, mbobevu wa Fizikia na Hisabati.

> Ilikuwa kipindi cha mpambano mkuu kwake, Dk Bilal katika mchakato wa awali kuwania urais Zanzibar, akaibuka katika nafasi ya juu ya walioomba kugombea urais.



Dk. Gharib Bilal akiwa na Ellen Johnson Sirleaf, Rais mstaafu wa Liberia.

Baada ya hapo akapata fursa kuendelea na elimu zaidi ya Fizikia alikopata shahada ya pili katika Chuo Kikuu cha California na akahitimu mwaka 1969. Baadaye, akaendelea na shahada yake ya uzamivu aliyohitimu mwaka 1976.

### ALIVYOHAMIA SIASA

Mwaka 1995, akahamia Zanzibar, ambako Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Salim Amour, akamteua Dk. Bilal kuwa Waziri Kiongozi, baada ya aliyekuwa katika nafasi hiyo, Dk. Omar Ali Juma, kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Serikali ya Jamhuri.

Dk. Bilal alifanya kazi hiyo kwa miaka mitano akiwa msaidizi mkuu wa Dk. Salim na akaonekana kukubalika katika siasa za Zanzibar, kiongozi wake Dk Salmin alipomaliza muda wake kuongoza Zanzibar kwa miaka 10, Dk. Bilali alionekana kukubalika, pale alijitosa kuvaa kiatu chake, ambacho hakubahatika kukipata.

Ilikuwa kipindi cha mpambano mkuu kwake, Dk Bilal katika mchakato wa awali kuwania urais Zanzibar, akaibuka katika nafasi ya juu ya walioomba kugombea urais.

Hata hivyo, matokeo ya mchakato huo mshindi kukwea nafasi hiyo ya kuwania urais alikuwa, Amani Abeid Karume, ambaye aligombea na kuwa Rais wa Zanzibar, mwaka 2000.

Baada ya hapo Dk. Bilal akabaki katika uanachama wa CCM na akitumikia bodi mbalimbali za taasisi za kawaida zikiwamo magazeti, pia taasisi za elimu ya juu.

Mwaka 2005 Dk Bilal akaibuka kuwa kivutio kwa umma, alipoenda kinyume na mazoea yaliyoko ndani ya chama chake, CCM katika mchakato wa kumpata mgombea urais. Hapo ni alipoamua kugombea urais wa Zanzibar, bila kusubiri kipindi cha pili cha uongozi wa rais aliyekuwepo kumaliza muda, hata kuibua mjadala kutoka kwa umma.

Chama chake kiliondoa mijadala na hata akashuhudiwa akiwa mgombea mwenza, katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010, hatua iliyomfanya Dk Bilali kuwa Makamu wa Rais kwa kipindi cha miaka mitano.

Akizungumza na Nipashe akiwa kwake unguja, katika maisha ya kuwa Makamu wa Rais Mstaafu, anasema moja ya mambo yaliyomgusa hata kuchukua fomu ya kugombea urais Zanzibar, ni kuwepo makundi mawili aliyoyashuhudia na alifanya hivyo, akiamini lilikuwa jambo sahihi wakati huo na hakuwa na vikwazo vya kiutaratibu.

Anaeleza, hata alipofika hatua hakufanikiwa kwa alichotaka, Dk. Bilal anaeleza akaheshimu matokeo hayo na utaratibu wa chama, kwa maana ya CCM na hata 'maisha yakasonga mbele.'

Kwa sasa, Dk. Bilal anajitambulisha ni mstaafu na amekuwa akionekana katika mikutano mbalimbali ya wataalamu wa sayansi na teknolojia.



## Balozi apanda mlima kumuunga mkono Rais

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIKA kuunga jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan kutunza mazingira na kutangaza utalii, Balozi wa Mazingira, Nestory Mushi, amepanda Mlima Kilimanjaro kwa lengo la kuunga mkono jitihada hizo.

Akizungumza na Nipashe jijini hapo jana, balozi huyo alisema ameamua kupanda mlima huo na kupeleka kileleni picha ya Rais Samia kutokana na dhamira yake njema ya kuhimiza masuala ya mazingira na kutangaza vivutio vya utalii vilivyoko nchini.

Mushi ambaye aliteuliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira kuwa Balozi wa Mazingira, alisema Rais Samia kupitia filamu ya Tanzania The Royal Tour, ametangaza vivutio vya utalii vya Tanzania, ukiwamo mlima huo.

"Katika safari yangu ya kupanda Mlima Kilimanjaro, nililenga kutoa elimu na hamasa kwa watalii na wasaidizi juu ya uhifadhi na utalii," alisema.

Alipoulizwa kuhusu eneo la mlima lililokuwa limeungua kwa moto mwaka jana kama uoto wake umeanza kurejea, balozi huyo alisema kwa sasa nyasi zimeanza kustawi na mazingira ya eneo hilo ni mazuri.

"Rai yangu kwa wahifadhi ni kuendelea kusimamia sheria za usimamizi wa hifadhi zote nchini. Nimeona kwa Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro mazingira yanatunzwa vizuri na hakuna utupaji taka ovyo," alitoa ushuhuda wake.

Alisema safari yake pia ililenga kutangaza shughuli za mabalozi wa mazingira nchini ambapo kwa siku zote alizokuwa akipanda mlima huo, alitoa elimu kwa watu takriban 100 kuhusu suala la mazingira.

"Suala la uhifadhi wa mazingira ni jukumu la kila mmoja kwa kutoa elimu na kujali mazingira yanayomzunguka," balozi huyo alihimiza.

Mlima Kilimanjaro unashika nafasi ya pili katika orodha ya milima mirefu zaidi duniani ukiwa na urefu wa mita 5,895, ukitanguliwa na Everest wenye urefu wa mita 8,848.

# Vituo vya malezi, makuzi ya awali watoto kujengwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI inapanga kuanzisha vituo vya malezi na makuzi ya awali ya watoto nchi nzima vitakavyotumika kutoa huduma hiyo bure kwa wazazi wasiokuwa na uwezo wa kulipia.

Kamishna Ustawi wa Jamii Msaidizi Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsi, Wanawake na Makundi Maalum, Baraka Makona, alibainisha hayo juzi jijini hapo alipofungua kongamano la miaka 25 la Montessori.

Makona alisema serikali imepanga kuja na mpango huo ambao utawezesha vituo hivyo kujengwa na kutoa fursa kwa wazazi kupeleka watoto wao bila malipo.

"Tunakuja na mpango mpya wa kujenga vituo vya kijamii vya kutoa huduma ya malezi na makuzi ya awali ili kutoa fursa kwa watu wote, hata wale wasiokuwa na uwezo wa kulipia katika 'Day care' za watu binafsi, watapata fursa. Hivi sasa vituo hivi vya kijamii vya serikali tunavyo 30 katika mikoa ya Dodoma na Dar es Saalam," alisema.

Kamishna huyo alisema kupitia Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano wa Malezi na Makuzi ya Awali ya Mtoto, serikali imejipanga kutoa elimu kupitia makundi mbalimbali ili kuwa na watoto wenye uelewa na wanaoweza kujisimamia.

Vilevile, alisema kupitia mpango huo, watatoa mafunzo kwa walimu, watoa huduma wa vituo vya afya pamoja na wazazi ili kujua namna bora ya kulea watoto.

"Watoto wa umri kuanzia miaka miwili hadi minane ndiyo umri ambao kama tutashindwa kuwajengea msingi wa malezi na makuzi, tutakuwa na watu wazima wazioweza kujisimamia wenyewe," alitoa angalizo.

Alisema kwa kuwa malezi yanagusa maeneo mengi, watatoa mafunzo kupitia mpango huo wa taifa kwa watoa huduma wa vituo vya afya kuelimisha wazazi namna ya kuzungumza na kulea watoto wao.

"Lazima wazazi wajue ni namna gani wanaweza kuzungumza na watoto wao pindi wanapokuwa na msongo wa mawazo, unaweza kukuta wakati mwingine mtoto ana msongo wa mawazo kutokana na kupigwa na mwenzie, sasa lazima kama mzazi uwe na njia uitumie ili kumfanya arudi katika hali yake badala ya kumfokea," alisema.

Alisema mpango huo pamoja na kutoa elimu katika makundi hayo, pia unalenga kutasaidia kupunguza vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

Mjumbe wa Kamati Tendaji ya Montessori, Kemilembe Ndyamukama, alisema Montessori ni mwanafalsafa ambaye alibaini zana za kujifunza watoto kulingana na mazingira wanakotoka.

"Tunapozungumzia mtoto tunazungumzia mtu mzima wa baadaye. Watoto katika hatua fulani ya makuzi wanakuwa na akili ya kufyonza kila mambo, hivyo kama atakuwa kwenye jamii ambayo inafanya vitu vya ovyo, mtoto anavyonza kila kitu bila kujali kuwa kina madhara kwake au la," alisisitiza.



Ofisa Idara ya Oganaizesheni Ofisi za Chama Cha Mapinduzi (CCM), Makao Makuu Dodoma, Neema Mfugale (kulia), akimkabidhi Judith Mollel, fomu ya kuomba kuteuliwa na chama hicho, kugombea ubunge wa Bunge la Afrika Mashariki, jijini Dodoma juzi. CCM wameanza kutoa fomu hizo kwenye ofisi zao za Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Katibu Mkuu ataka utunzaji mradi mabadiliko tabianchi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), amewataka wakazi wa Wilaya ya Mpwapwa kuutunza Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mifumo Ikolojia (EBBAR) ili ulete matokeo chanya kwenye mazingira.

Dk. Switbert Mkama alitoa rai hiyo juzi wakati wa ziara ya kikazi ya kukagua utekelezaji wa mradi huo unaotekelezwa wilayani Mpwapwa.

Kiongozi huyo alisema wananchi wanao wajibu wa kutunza na kusimamia kikamilifu miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao.

"Leo (juzi) nimeshuhudia kukamilika kwa visima virefu vinne vyenye uwezo wa kutoa lita 40,000 kwa siku ambavyo vinanufaisha wakazi wa vijiji vya Nghambi, Mbugani, Kiegea na Kazani.

"Serikali inatafuta fedha za kutekeleza miradi hii yenye faida kubwa kwa wananchi. Ninatoa rai kwenu muitunze, iwasaidie na kuleta manufaa sasa na kwa vizazi vijavyo," aliagiza.

Aliwataka wanufaika wa miradi hiyo kuongeza kasi ya upandaji miti katika maeneo yao na kujishughulisha na kilimo rafiki kwa mazingira kama chanzo mbadala cha kujiongezea kipato.

Diwani wa Ng'hambi, Richard Milimo, alibainisha kuwa mradi huo umekuwa mkombozi kwa wakazi hao kwa kuwa umetatua tatizo la maji lililokuwa likiwakabili kwa muda mrefu.

"Sh. milioni 800 zimetumika kupitia mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia mifumo ikolojia ambapo mipango ya matumizi ya ardhi imeandaliwa, visima virefu vinne, malambo mawili, majosho mawili, vitalu nyumba vitatu na mashine ya kukamulia alizeti vimepatikana kupitia utekelezaji wa mradi huu unaosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais," alisema.

Mradi huo pia unatekelezwa katika Halmashauri za Kaskazini A (Unguja), Simanjiro (Manyara), Mvomero (Morogoro) na Kishapu (Shinyanga).

Kwa sasa dunia inashuhudia athari nyingi za mabadiliko ya tabianchi, baadhi yake ni joto na baridi kali pamoja na ukame katika baadhi ya maeneo.





# Taasisi yaja na mtaala maalumu kilimo nchini

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kahawa (TaCRI) imeandaa mtaala maalum uliosheheni mafunzo, teknolojia na elimu kwa lengo la kuwapatia wakulima mbinu kunufaika na kilimo cha zao hilo kwenye maonesho ya wakulima, maarufu Nanenane yanayofanyika kitaifa katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya.

Meneja wa Programu za Utafiti TaCRI Kanda ya Mbeya, Dk. Dismas Pangalasi, alibainisha kuwapo mkakati huo jana alipozungumza na Nipashe kuhusu mikakati waliyojiwekea katika kuhakikisha teknolojia na elimu kuhusu zao hilo inawafikia wakulima.

Dk. Pangalasi alisema mtaala huo wa mwongozo na mafunzo utakuwa unatolewa na wataalamu wa TaCRI kwa wakulima ambao watakuwa wanatembelea banda hilo kwenye maonyesho hayo.

"Nanenane ya mwaka huu tumekuja na mtaala wa kufundishia zao la kahawa ambao wataalamu wetu watakuwa wanawafundisha wakulima miongozo mbalimbali ya namna wanapaswa kufuatilia ili kupata tija kwenye zao la kahawa," alisema.

Dk. Pangalasi aliongeza kuwa wamejipanga kuonyesha aina 19 za mbegu bora aina ya rabika ambayo imebuniwa nchini na taasisi hiyo, akitamba ina sifa mbalimbali kama vile kuwa na vionjo tofauti kulingana na mahitaji ya soko la dunia pamoja na virutubisho.

Alisema pia waleta mbegu nyingine mpya tatu aina ya chotara ambazo alisisitiza zinafanya vizuri kwa kuzalishaji mavuno mengine na kuhimili hali ya hewa ya ukanda wa nyanda za juu kusini.

Alisema mbegu hizo ni miongoni mwa zilizobuniwa katika kipindi cha miaka 19 ya utafiti uliofanywa na TaCRI na kusaidia hadi sasa kupata aina 24 za mbegu zilizobuniwa.

Dk. Pangalasi alisema wamedhamiria kuwafikia wakulima 8,000 hadi 10,000 wa kahawa kutoka maeneo mbalimbali nchini ambao watafundishwa namna ya kutoa huduma za zao la kahawa ili kuleta tija na uzalishaji utaochangia ukuaji wa pato kwa mkulima.

"TaCRI tunajivunia mafanikio ya utafiti wetu ambapo kwa kipindi cha miaka 19 tumefanikiwa kugundua aina 19 bora za kahawa arabika na aina tano za rubusta ambazo zimekuwa zikifanya vizuri sana kwa wakulima wetu.

"Vilevile, tumefanikiwa kufanya upembuzi yakinifu wa afya ya udongo nchi nzima kwa kuandaa makala na taarifa mbalimbali zinazoelezea mahitaji ya virutubisho katika kila kipande cha ardhi," alisema Dk. Pangalasi.

Alitaja vikwazo wanavyokabiliana navyo ni pamoja na uhitaji mkubwa wa miche ya kisasa kulinganisha na uzalishaji uliopo.

Alisema mahitaji ya miche ya kahawa ni makubwa kuliko uzalishaji wenyewe kutokana na ukata wa fedha, hali inayosababisha wakulima kushindwa kulima mazao ya kutosha.

Kutokana na hali hiyo, aliiomba serikali na wadau wengine kuendelea kuwapatia fedha kwa ajili ya kuzalisha miche mingi itakayokidhi mahitaji ya wakulima na kuongeza uzalishaji.

Maonyesho hayo yalizinduliwa rasmi juzi na Makamu wa Rais, Dk. Mpango juzi.




Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anney (kushoto), akijadiliana jambo na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya TOL Gases Ltd, Daniel Warungu, katika uzinduzi wa kiwanda kipya cha gesi cha TOL Kijiji cha Ikama wilayani humo, mkoani Mbeya mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TARI yapewa jukumu la kumaliza udumavu

**Na Ashton Balaigwa,** MBEYA

SERIKALI imeagiza Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kufanya utafiti na kuja na majibu ya mbegu zitakazokuwa na viini lishe na vitamini ili kusaidia kumaliza tatizo la udumavu wa watoto ambalo kwa sasa limekuwa ni tishio nchini.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alitoa agizo hilo juzi alipozungumza na watafiti wa TARI alipotembelea banda lao kwenye maonyesho ya wakulima na wafugaji yanayofanyika kitaifa katika viwanja vya John Mwakangale mkoani hapo.

Dk. Mpango alitoa agizo hilo baada kupewa taarifa na Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geoffrey Mkamilo, kuwa watafiti wa taasisi hiyo Kituo cha Uyole mkoani Mbeya wamegundua mbegu ya maharagwe yenye viini lishe na zinki inayosaidia kuimarisha afya kwa watoto na watu wazima.

Akizungumza na watafiti hao, Makamu wa Rais alisema bado kuna tatizo la udumavu nchini ambalo lipo katika mikoa ambayo inalima chakula kwa wingi.

"Kuna tatizo la udumavu sana kwa watoto hata kwenye mikoa inayolima chakula kwa wingi, hivyo tunataka ninyi watafiti mfanye utafiti wa mazao yatakayozalishwa yawe na vitamini na viini lishe kusaidia kumaliza udumavu," alisema.

Makamu wa Rais pia aliionya Wizara ya Kilimo kuacha kuzikalia fedha za utafiti, akisema bila utafiti, itakuwa ngumu kuinua kilimo nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Mkamilo, alisema agizo hilo litafanyiwa kazi na watafiti ili kulisaidia taifa kuondokana na udumavu hasa kwa watoto.

Dk. Mkamilo alisema TARI kupitia vituo vyake vya utafiti vilivyoko nchini, imebaini mbegu bora za mazao mbalimbali na kuzifanyia majaribio katika maeneo mbalimbali na kuonyesha mafanikio.

## Bodi ya Mazao yataja bidhaa pendwa sokoni

**Na Renatha Msungu,** MBEYA

BODI ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) imeanza kujenga mtandao mkubwa wa kutafuta masoko ya bidhaa kwenye nchi za Afrika Mashariki ili kuhakikisha wakulima wananufaika na kilimo wanachofanya.

Vilevile, imehimiza wakulima kujikita katika kilimo cha alizeti, soya na mtama mweupe kutokana na bidhaa hizo kuwa na soko kubwa ndani na nje ya nchi.

Mkurugenzi Mkuu wa CPB, Dk. Anslem Moshi, alibainisha hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari kwenye viwanja vya maonyesho ya kitaifa ya wakulima, maarufu Nanenane, yanayoendelea jijini Mbeya.

Dk. Moshi alisema lengo la bodi hiyo kufanya hivyo ni pamoja na kutaka kuwainua wakulima kiuchumi kupitia kilimo, pia wapate fursa ya kufanya biashara nje ya nchi.

"Tumepanua wigo kwa kutafuta masoko nje ya nchi, tunafanya hivyo ili kukuza soko la bidhaa zetu," alisema Dk. Moshi. Alizitaja baadhi ya nchi ambazo wana masoko ya bidhaa za nafaka ni pamoja na Uganda, Kenya, Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Mbali na hilo, aliwataka wajasiriamali wa vifungashio, usindikaji na wengine kutumia fursa iliyotolewa na bodi ya kuingia mkataba wa kufanya kazi nao ili kuviboresha zaidi.

Alisema bodi hiyo inafanya kazi mbalimbali ikiwamo kusafirisha mazao, hivyo akawataka wakulima kutokuwa na wasiwasi wowote wanapohitaji kupata huduma hiyo.

Alisema wakulima wanapaswa kuitumia CPB ili kuboresha bidhaa wanazozolima na baadaye kuzipeleka sokoni ili ziwe na kiwango bora kabla ya kuuzwa.

Mkurugenzi huyo wa CPB alisema wajasiriamali wanaotaka kutumia fursa hiyo, wajitokeze kwa wingi ili wakae pamoja kuona namna ya kushirikiana ili wasonge mbele katika kuziboresha bidhaa hizo.

"Tumetoa fursa ya kufanya kazi na wajasiriamali kwa wale wanaohitaji, mje CPB, iwe wa kusindika, kutengeneza vifungashio na wengine mnakaribishwa," alisema.

Akizungumzia kuhusu kilimo cha mtama mweupe, alizeti na soya, mkurugenzi huyo alisema wakulima wanapaswa kulima kwa wingi kwa sababu mazao hayo kwa sasa yana soko kubwa ndani na nje ya nchi.

Mkulima Elia Atupele alisema amenufaika na bodi hiyo kutokana na kuuza mazao mbalimbali kwenye bodi hiyo na hata kusaidiwa kupata masoko kirahisi.



## Mwinyi apongeza utendaji wa JWTZ

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amelipongeza Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kwa kuendelea kusimamia vizuri ulinzi na usalama nchini.

Alitoa pongezi hizo jana Ikulu Zanzibar alipozungumza na Mnadhimu Mkuu wa Jeshi hilo, Luteni Jenerali Salum Haji Othman, aliyefika Ikulu kwa ajili ya kujitambulisha.

Dk. Mwinyi alisema hali ya amani, ulinzi na usalama Zanzibar imezidi kuimarika kutokana na kuwapo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Alisema jeshi hilo lina mchango mkubwa katika mafanikio hayo kutokana na jitihada zake katika kusimamia ulinzi na usalama wa nchi.

Rais Dk. Mwinyi amemhakikishia Mnadhimu Mkuu huyo kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kushirikiana na jeshi hilo ili mafanikio zaidi yapatikane.

Alimpongeza Luteni Jenerali Othman kwa kuteuliwa kushika wadhifa huo na kumwahidi kwamba ataendelea kushirikiana naye ili aendelee kufanya kazi zake katika kulitumikia jeshi hilo kwa ufanisi zaidi. Dk. Mwinyi pia alisema ipo haja ya kuendeleza ushirikiano na Chuo cha Ulinzi cha Taifa (NDC) na kuahidi kwamba Serikali ya Zanzibar itaendeleza ushirikiano na chuo hicho ambacho kila mwaka wahitimu wake hufika Zanzibar ikiwa ni sehemu yao ya masomo.

Mnadhimu Mkuu wa JWTZ, Luteni Jenerali Othman, alisema uteuzi wake katika nafasi hiyo ulifanyika Juni 30, mwaka huu, baada ya aliyekuwa Mnadhimu Mkuu Luteni Jenerali Mathew Mkingule kupangiwa majukumu ya ubalozi Zambia.

Alisema kutokana na kuteuliwa kwake, ameona ni vyema afike Ikulu kumsalimia Rais pamoja na kujitambulisha kwake na kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mnadhimu Mkuu huyo alieleza jinsi anavyotambua mchango mkubwa wa Rais Dk. Mwinyi pamoja na serikali yake kwa JWTZ.

"Mheshimiwa Rais, umekuwa karibu sana na jeshi letu kwa ushauri na kwa nasaha zako zilizojaa hekima na busara nyingi ulizojaaliwa na Mwenyezi Mungu. JWTZ siyo taasisi ngeni kwani kupitia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa umeliongoza jeshi hili kwa miaka 10. "Katika mazingira haya, sidhani kama kuna jambo jipya nitakaloweza kukueleza ukawa hulifahamu kuhusu JWTZ na sekta nzima ya ulinzi kwa ujumla wake," alisema.

Luteni Jenerali Othman alieleza jinsi Rais Dk. Mwinyi kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar anavyosaidia kwa kiasi kikubwa katika kuleta utangamano kati ya wananchi na jeshi lao kuhusu masuala mbalimbali ikiwamo migogoro ya ardhi na kusaidia kupata ufumbuzi wa kudumu.

# USAID yatakiwa kupanua wigo uhuishaji wa miradi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar amelitaka Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID) kupanua wigo wa uhuishaji wa miradi inayojumuisha uchumi wa bu-luu.

Hemed Suleiman Abdullah alitoa rai hiyo jana, wakati akifunga mradi wa Inua Vijana uliofadhiliwa na shirika hilo mjini Zanzibar.

Makamu wa Rais alilitaka shirika hilo kuwapa kipaumbele wanawake katika upatikanaji wa ruzuku na kujenga mnyororo wa thamani kwenye sekta ya hoteli na kuhakikisha chakula kinazalishwa na kuuzwa ndani ya nje ya nchi.

Alisema ni aibu muhogo kuagizwa nje ya Zanzibar hasa wakati wa mwezi wa Ramadhan ambapo kipindi hicho zao hilo hutumika kwa wingwi wakati Zanzibar ina uwezo wa kuzalisha zao hilo.

Hemed alisema serikali itaendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo ili kuhakikisha inatimiza dira na dhamira ya maendeleo kama mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar inavyojielekeza zaidi katika viashiria vya uchumi jumuishi na mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo Zanzibar kwa mwaka 2022/2023.

Alisema kuwa hayo yanapaswa kutekelezwa kwa kuzingatia vipaumbele vya serikali vilivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050.

Alisema serikali zote mbili kwa kushirikiana na Serikali ya Marekani kupitia USAID, zimewezesha kuwajengea uwezo vijana wa Tanzania kuwa nguvu kazi ya taifa na kuleta maendeleo chanya kwa kuwapa elimu ya ujasiriamali na mafunzo ya stadi za maisha.

"Kupitia mradi huu, vijana wamepata fursa za masoko na mitaji ya kuendeleza biashara zao. Ni matumaini yangu vijana mtaendelea kuutumia ujuzi, maarifa na stadi mlizopata katika kuongeza ajira zaidi kwa kujiajiri ili kupunguza kiwango cha umaskini na hatima ya mafanikio ya nchi yetu imo mikononi mwenu," alihimiza.

USAID imetoa ruzuku ya Sh. bilioni 9.6 kupitia mradi huo kwa kuwafikia vijana 44,000 katika kipindi cha miaka mitano.

Balozi wa Marekani nchini, Donald Wright, alisema mradi huo umewafikia zaidi ya vijana 40,000 na kutoa rukuzu ya Sh. bilioni 5.3 kwa miradi ya kilimo biashara inayosimamiwa na vijana.

Alisema mradi pia umetengeneza vikundi vya kuweka na kukopa vyenye wanachama vijana zaidi ya 6,000 vikiwa na thamani ya Sh. bilioni 2.7.

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Muhammed Said, alisema mradi huo ni kianzio cha safari kwa vijana katika kuyafikia masoko, yakiwamo yaliyoko katika sekta ya utalii kwa kusambaza bidhaa zao kwenye hoteli za kitalii Zanzibar.

Alisema ni lazima kuhakikisha bidhaa zote zinazozalishwa na wajasiriamali, zikiwamo bidhaa za mboga na matunda, zinapata soko Zanzibar.

Waziri wa Kilimo, Mifugo na Umwagiliaji, Shamata Shaame Khamia, alisema wizara yake itaendelea kutoa ushirikiano ili nguvukazi hiyo ya vijana iendelee kukuza uchumi.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Abeda Rashid (kushoto), akizungumza na wajasiriamali wanaopatiwa mafunzo ya utengenezaji wa bidhaa mbalimbali ikiwamo sabuni ili kujikomboa kiuchumi, jijini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wajasiriamali wapewa mikopo nafuu serikalini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea kuwawezesha wajasiriamali wadogo kwa kuwapatia mikopo nafuu ili wajikwamue kiuchumi.

Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Maryam Juma Sadala, alibainisha hayo jana wakati wa ziara ya kuvitembelea vikundi vya wajasiriamali wadogo huko Kijichi na Masingini, nje kidogo ya Mji wa Zanzibar.

Alisema serikali imetenga Sh. bilioni 31 kwa ajili ya kutoa mikopo hiyo kupitia Benki ya CRDB, hatua itakayowakwamua kiuchumi.

Alisema lengo la kuvitembelea vikundi hivyo ni kuvifanyia tathmini, kuvisaidia kuandika maandiko ya miradi na kupata ujuzi ili kukidhi kupata mikopo hiyo kwa manufaa ya baadaye.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum, Dk. Zainab Abdi Chaula, alivitaka vikundi hivyo kushirikiana na serikali kuendeleza kazi zao wakati serikali ikiimarisha mazingira bora ikiwamo masoko na vitendea kazi.

Mkurugenzi Msaidizi wa Wizara hiyo, Badru Abdu, alisema lengo ni kuwasaidia wajasiriamali hao, hasa wanawake walio kwenye vikundi, wakue kiuchumi.

Alisema hatua hiyo ni kutekeleza ahadi ya Rais Samia Suluhu Hassan na Rais Dk. Hussein Mwinyi kuweka mipango imara ya kulikuza kundi hilo kiuchumi.

Baadhi ya wanawake waliokuwamo katika vikundi hivyo vya ushirika, walitaja baadhi ya vikwazo vinavyowakabili ikiwa ni pamoja na ukosefu wa fedha na vitendea kazi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA

**IDDI ATHUMAN NDAKI** anatangaza kupotelewa na Offer Letter ya kiwanja ILALA UTETE STREET HOUSE NA. **8 PLOT NA. 19** BLOCK NO. **0000 7402 DAR ES SALAAM.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/TAB/RB/294137/2022.**

---

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MASWA LILILOPO MASWA**
**MAOMBI MAKUBWA NA. 40 YA MWAKA 2022 NA MAOMBI MADOGO NO. 800 YA MWAKA 2022**
**KATI YA**
**ROBERT PAULINE......................MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**ELEN ELIAS..........................MJIBU MAOMBI**

**WITO/TAARIFA**

**KWA: ELEN ELIAS – POPOTE ALIPO KATIKA JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

Kwa kuwa mwombaji hapo juu amefungua maombi dhidi yako katika Baraza hili la Wilaya ya Maswa, maelezo ya madai yanaweza kupatikana hapa Barazani. Unatakiwa kuleta hapa Barazani utetezi wa maandishi (WSD) kabla ya tarehe 1/9/2022. Pia unajulishwa kuwa shauri hili limepangwa kutajwa siku ya tarehe 1/9/2022 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh. J.T. Kaare Mwenyekiti, Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Maswa. Na pia unafahamishwa kuwa iwapo utakaidi wito huu na kushindwa kutoa utetezi wa maandishi kwa muda uliopangwa, Baraza litalazimika kusikiliza shauri hili upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yako.
IMETOLEWA kwa MKONO wangu na MHURI wa Baraza hii leo tarehe 27/7/2022.

J.T.KAARE
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) MASWA

MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MASWA TANZANIA

---

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MASWA LILILOPO MASWA**
**MAOMBI MAKUBWA NA. 42 YA MWAKA 2022 NA MAOMBI MADOGO NO. 800 YA MWAKA 2022**
**KATI YA**
**CHARLES PETER......................MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**ELIZABETH MASALU..........................MJIBU MAOMBI**

**WITO/TAARIFA**

**KWA: ELIZABETH MASALU – POPOTE ALIPO KATIKA JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

Kwa kuwa mwombaji hapo juu amefungua maombi dhidi yako katika Baraza hili la Wilaya ya Maswa, maelezo ya madai yanaweza kupatikana hapa Barazani. Unatakiwa kuleta hapa Barazani utetezi wa maandishi (WSD) kabla ya tarehe 25/08/2022. Pia unajulishwa kuwa shauri hili limepangwa kutajwa siku ya tarehe 25/08/2022 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh. J.T. Kaare Mwenyekiti, Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Maswa. Na pia unafahamishwa kuwa iwapo utakaidi wito huu na kushindwa kutoa utetezi wa maandishi kwa muda uliopangwa, Baraza litalazimika kusikiliza shauri hili upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yako.
IMETOLEWA kwa MKONO wangu na MHURI wa Baraza hii leo tarehe 22/7/2[illegible]

J.T.KAARE
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) MASWA

MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MASWA TANZANIA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA KIHONDA**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......39/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: FATUMA RASHID WA MAFISA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**YALIYOLETWA NA HUSSEIN SHOMARY MWINYIMBEGU**

**TANGAZO**

(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 10 Mwezi 08 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 02 mwezi 08 mwaka 2022**

HAKIMU

**HAKIMU MFAWIDHI**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MJINI MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......43/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: OCTAVIAN LEO MAGWILA WA MBIGILI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**YALIYOLETWA NA AUGUSTINA LEO MAGWILA**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 15 Mwezi 08 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 01 mwezi 08 mwaka 2022**

**HAKIMU MFAWIDHI**

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**AMYE SIVALI** anatangaza kupotelewa na cheti cha **FORM FOUR (CSEE)** chenye **INDEX NO: S 0311 – 005** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **FORODHANI SECONDARY SCHOOL MWAKA: 1993. CHETI CHA FORM SIX (ACSEE)** chenye **INDEX NO: S 0350 – 0501** kilichotolewa na **SHINYANGA COMMERCIAL INSTITUTE MWAKA 1996. PAMOJA NA CHETI CHA DARASA LA SABA. TAARIFA YA UPOTEVU ILITOLEWA KATIKA KITUO CHA POLISI CHA CENTRAL NA KUPEWA RB NO: DAR /CEN/RB/304134/2022.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**AMYE SIVALI** anatangaza kupotelewa na **CHETI CHA CHUO - ADVANCED DIPLOMA IN ACCOUNTANCY chenye REG NO: TFC 97/ ADA cha COLLEGE OF BUSSINESS EDUCATION MWAKA 2001. CHETI CHA CHUO - DEGREE OF MASTER OF BUSINESS ADMINISTRATION (SN NO: 2163) cha MZUMBE UNIVERSITY MWAKA: 2010. CHETI CHA CHUO - COMPLEXION OF THE CERTIFIED PUBLIC ACCOUNTANT CPA (T)** chenye namba **NBAA / CR NO. 0006484 (SERIAL NO: 5583)** cha **THE NATIONAL BOARD OF ACCOUNTANTS AND AUDITORS - MWAKA 2016. TAARIFA YA UPOTEVU ILITOLEWA KATIKA KITUO CHA POLISI CHA CENTRAL NA KUPEWA RB NO DAR / CEN /RB/304134/2022.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ABDALHAMID KANGETA ISMAIL ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA CARINA YENYE NAMBA ZA USAJILI T 615 BAU. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI KAH/RB/495/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BARAKA PETER GEORGE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA SURF** yenye namba za usajili **T910BLQ.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/257240/2022.**

## KUFUNGA KAMPUNI

WAMILIKI EZEKIEL JAPHET SAGASII & CATHERINE JAPHET MUOJERWA WA KAMPUNI YA REMIMA BUSINESS COMPANY LTD YENYE USAJILI NO 133686 MNAMO TAREHE 30/03/2021, WANAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA KAMPUNI YAO HAIJAKIDHI VIGEZO VYA BOT YA KUBADILI JINA LA BIASHARA LIWEZE KUSOMEKA MICROFINANCE HIVYO KUAMUA KUIFUNGA KWA MUJIBU WA SHERIA YA MAKAMPUNI BRELA

EZEKIEL JAPHET SAGASII
DIRECTOR

CATHERINE JAPHET MUOJERWA
MANAGING DIRECTOR

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HALIMA I. KAPILIMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina **MOHAMED ENTERPRISES** aina ya **BOXER** yenye namba za usajili **MC266CKQ.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/291367/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Kihonda**
**Wilaya ya Morogoro**
**Mkoa Wa Morogoro**
**Usimamizi wa Mirathi......21..2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU**
**SHABAN H MHANDO WA M/SONGO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA SAIDI IDDI KINYOGOLI**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 24/03 /2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe 17/03/2022**

KNY. MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO

---

***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku***

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Marekani yamuua kiongozi wa Al-Qaida

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Joe Biden, ametangaza kuwa kiongozi mkuu wa kundi la al-Qaida Ayman al-Zawahiri ameuawa na mashambulizi ya ndege yao isiyo na rubani mjini Kabul Afghanistan huku Saudi Arabia ikisifia.

Akizungumzia kutokea Ikulu ya White House usiku wa kuamkia jana Biden aliitaja operesheni iliyomuua Zawahiri mjini Kabul kwamba imetenda haki na italeta faraja kwa familia za waathirika wa mashambulizi ya Septemba 11, mwaka 2001 nchini Marekani.

Mbali ya mashambulizi hayo ya Septemba 11, Biden alitumia sababu nyengine ya ziada kuhalalisha uamuzi wake wa kuamuru mauaji ya Zawahiri baada ya siku chache zilizopita kuwataka wafuasi wake kuishambulia Marekani.

"Alifanya video zikiwamo za wiki za hivi karibuni, akiwataka wafuasi wakeu dhidi ya wale wanaotaka kuwadhuru, nasisitiza tena haijalishi itachukua muda gani ikiwa wewe ni tishio, tutakutafuta na tutakupata," alisema.

Kwa mujibu wa duru za kiusalama, Biden aliidhinisha mashambulizi hayo ya ndege zisizo na rubani aina ya Hellfire Julai 25 wakati akiwa anaendelea kujiuguza maambukizo ya virusi vya UVIKO-19 na kwamba Zawahiri aliuawa asubuhi ya Julai 31 akiwa amekaa kwenye baraza ya nyumba yake katika mtaa mmoja wa

Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje ya Saudia, mzaliwa huyo wa Misri, anachukuliwa kama mmoja kati ya viongozi wa ugaidi aliyepanga na kuongoza operesheni za kigaidi ndani ya Marekani, Saudi Arabia na mataifa mengine duniani. **DW**



**Biden aliitaja operesheni iliyomuua Zawahiri mjini Kabul kwamba imetenda haki na italeta faraja kwa familia za waathirika wa mashambulizi ya Septemba 11, mwaka 2001 nchini Marekani.**




Mgombea urais nchini Kenya, Raila Odinga. **PICHA: MTANDAO**

# Majukumu ya IEBC kuelekea uchaguzi Kenya

**NAIROBI,** Kenya

KUELEKEA uchaguzi mkuu nchini Kenya utakaofanyika Jumanne wiki ijayo, macho na masikio sasa ni kwa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka IEBC kuhakikisha kuwa zoezi hilo linakuwa huru na haki.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na RFI, IEBC ilibainsha kuwa mipango yote imakamilika kutoa nafasi kwa wapigakura zaidi ya milioni 22 kufanya maamuzi kuhusu nyadhifa mbalimbali za uteuzi hasa ule wa urais.

Baada ya Kenya kupata Katiba mpya mwaka 2010, IEBC ni miongoni mwa Tume Huru zilizoanzishwa ili kusimamia uchaguzi huru na haki, baada ya vurugu za mwaka 2007.

Kwa mujibu wa IEBC wapigakura watahitajika kwenda katika vituo zaidi ya 46,000 ili kupiga kura, pia mbali na kumchagua rais, watawachagua magavana, maseneta, wabunge, wawakilishi wa wanawake na wale wa wadi.

Ilisema maofisa wa tume hiyo, watawatambua wapigakura kwenye daftari la kupigia kura kwa njia ya kielektroniki au ya kawaida, baada ya kuwasilisha kitambulisho cha taifa au pasipoti aliyotumia kujiandikisha kupiga kura.

Taarifa inaeleza kuwa tume hiyo inaongozwa na mwenyekiti na makamishna wengine na kazi yake itakuwa ni kuhakikisha zoezi limeenda vema na kumtangaza mshindi wa kinyang'anyiro cha urais.

**Baada ya kurejea nchini kwake aliendeleza harakati za kupigia siasa za vyama vingi na mara ya kwanza kuwania urais, ilikuwa mwaka 1997 na kuwa wa tatu kwa wingi wa kura.**

Aidha, IEBC ambayo ni mwamuzi wa uchaguzi huo, ina jukumu la kuhakikisha kuwa mshindi wa urais anakidhi viwango vya kikatiba kwa kupata asilimia 50 ya kura zote na angalau asilimia 25 katika kaunti 24 kati ya 47 nchini humo.

Kwa mujibu wa katiba ya nchi hiyo inatoa mpaka siku saba kwa tume ya uchaguzi kumtangaza mshindi toka siku ya upigaji kura.

### JITIHADA ZA ODINGA

Mmoja wa wagombea wakuu wa kinyang'anyiro hicho cha urais, Raila Odinga (77) amejitosa tena kwa mara ya tano kutafuta urais wa nchi hiyo ambapo anawania kupitia muungano wa kisiasa wa Azimio la Umoja One Kenya, na iwapo atafanikiwa kuingia Ikulu atakuwa rais wa kwanza kushika madaraka akiwa na umri mkubwa.

Vile vile Odinga anaingia katika vitabu vya siasa nchini Kenya, kama kiongozi wa upinzani wa muda mrefu anayeungwa mkono na rais anayeondoka madarakani, Uhuru Kenyatta baada ya wawili hao kupatana baada ya uchaguzi wa mwaka 2017.

Odinga ambaye wafuasi wake, humwita Baba, amekuwa na safari ndefu ya kisiasa, tangu kipindi cha harakati za vyama vingi nchini Kenya miaka ya 90, na kabla ya hapo, alifungwa jela kwa miaka sita kwa madai ya kushiriki njama ya kutaka kuipindua serikali ya aliyekuwa Rais Hayati Daniel Arap Moi mwaka 1982.

Pamoja na madai hayo lakini hakuwahi kupatikana na kosa na baadaye akaikimbia nchi mwaka 1991 baada ya kuachiwa huru.

Baada ya kurejea nchini kwake aliendeleza harakati za kupigia siasa za vyama vingi nchini Kenya na mara ya kwanza kuwania urais, ilikuwa mwaka 1997 na kuwa wa tatu kwa wingi wa kura.

Alijaribu tena mwaka 2007, 2013 na 2017 na nyakati zote alishika nafasi ya pili kwa wingi wa kura. Hata hivyo, uchaguzi wa mwaka 2007 uliishia kwenye machafuko ya kisiasa, baada ya kudai kuibiwa kura, hali iliyosababisha kuundwa kwa serikali ya muungano na kuhudumu kama Waziri Mkuu.

Wafuasi wake wanamsifia kama kiongozi mpenda haki na kiongozi anayependa kuongoza mageuzi kwa ajili ya wanyonge lakini wapinzani wake wanamwona kama mwanasiasa, asiyeridhika na anayependa kuihangaisha serikali iliyo madarakani. **RFI**

# SPORTPESA YASAINI MKATABA WA KUIDHAMINI SINGIDA BIG STARS FC

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Burudani na Michezo ya SportPesa, imetangaza kuingia rasmi mkataba wa miaka minne na Klabu ya Singida Big Stars kama mdhamini mkuu kwa mara nyingine kuanzia msimu huu wa mwaka 2022/23 mpaka msimu wa 2025/26.

Hafla hiyo ya kutambulisha mdhamini mkuu ilifanyika jana kwenye ofisi za SportPesa, Oysterbay jijini Dar es Salaam ikihudhuriwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa, Tarimba Abbas na kutoka Singida Big Stars wakiwakilishwa na Mkurugenzi Uendeshaji Masoko na Fedha wa klabu hiyo, Kanu Muhibu pamoja na baadhi ya wachezaji wa kikosi hicho chenye makao yake makuu mkoani Singida.

Akizungumza na waandishi wa habari katika hafla hiyo, Tarimba alisema azma ya SportPesa ni kuona soka la Tanzania linapiga hatua na kwenda mbele kwenye ushindani wa juu zaidi kwa kuchangia sekta hiyo na kwamba udhamini wanaoutoa kwa Singida Big Stars ni kutimiza nia yao ya siku zote tangu wameanza biashara hapa nchini.

"Kama mtakumbuka tangu tumeanza biashara mwaka 2017, tulianza na dhamini wa klabu pamoja na miradi mbalimbali ya kuinua soka la Tanzania. Hawa Singida Big Stars, zamani Singida United, tuliwadhamini wakati ule kwa mkataba wa mwaka mmoja. Leo tunatangaza kuwadhamini tena, kwa mkataba wa miaka minne, kuanzia msimu huu wa ligi, unaoanza hivi karibuni," alisema.

Kwa upande wa Singida Big Stars, Mkurugenzi wa Uendeshaji, Masoko na Fedha, Muhibu aliwashukuru SportPesa kwa kukubali kuwa wadhamini wao wakuu na pia kwa kuwa mstari wa mbele kwenye kukuza mpira wa miguu katika nyanja mbalimbali.

"Napenda kukukushukuru Tarimba kwa kuwa bega kwa bega na timu za Tanzania na pia kuwashukuru SportPesa kwa namna mnavyojitoa kusaidia katika kukuza na kuendeleza mpira Tanzania. Leo ni siku ya kipekee kwetu kusaini mkataba huu na pia kumtambulisha mdhamini wetu SportPesa ambaye ametupa mkataba mrefu wa miaka minne," alisema Muhibu.

Alihitimisha kwa kuahidi kwamba watasimamia vipengele vyote kama vilivyoainishwa katika mkataba na kuhakikisha wanapata matokeo ambayo yatakuwa chachu ya kuendeleza biashara na mahusiano baina yao.

"Mimi kama kiongozi katika timu, pamoja na watendaji wengine wote wa Singida Big Stars, ninaahidi tutatoa ushirikiano wa kutosha katika kutimiza, kufanikisha yale yote yaliyomo ndani ya mkataba huu. Kwa leo sina mengi sana zaidi ya kuwashukuru SportPesa pamoja na vyombo vya habari ambavyo vimekuwa nasi siku zote.

Hata hivyo, pande hizo mbili hazikuwa tayari kuweka hadharani thamani halisi ya mkataba huo wa miaka minne kwa sasa.




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa, Tarimba Abbas (kulia) na Mkurugenzi Uendeshaji Masoko na Fedha wa Klabu ya Singida Big Stars, Muhibu Kanu, wakionyesha mkataba wa udhamini jana jijini Dar es Salaam, baada ya kampuni hiyo michezo ya kubashiri kuidhamini klabu hiyo kwa mkataba wa miaka minne kuanzia msimu huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Simba kurejea kesho, yaacha kipigo Misri

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupiga kambi yake nchini Misri kwenye mji wa Ismailia kwa ajili ya msimu mpya, kikosi cha Simba kinatarajia kurejea nchini kesho mchana, huku kikiacha kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Al Kholood Club ya Saudi Arabia.

Akizungumza jana, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema baada ya mchezo huo uliofanyika juzi usiku Ismailia, jana kiliendelea na mazoezi yake na leo asubuhi kitafanya mazoezi, kabla ya kuondoka nchini humo usiku na kesho mchana kutarajiwa kuwasili, Dar es Salaam.

"Baada ya mchezo wa jana (juzi) dhidi ya Al Kholood, tutafanya mazoezi leo (jana) na tarehe tatu asubuhi, usiku kikosi kitaanza safari ya kurejea nchini na kinatarajia kuwasili nchini mchana na tarehe nne ambapo wachezaji wetu wataruhusiwa kidogo kwenda kusalimia familia, tarehe tano wataingia tena kambini kwa ajili ya kuelekea kwenye kilele cha Simba Day.

Wale wachezaji ambao hawakupata nafasi ya kujiunga kambini nchini Misri waliokuwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars, na wenyewe watajiunga na wenzao, sasa hapo mwalimu Zoran Maki, atakuwa na kikosi chake chote kikiwa kimekamilika," alisema Ahmed.

Katika mechi iliyochezwa juzi, mabao ya Simba yalifungwa na Gadiel Michael, huku mfungaji huyo pia akitoa pasi ya mwisho kwa Augustine Okrah aliyepachika bao la pili.

Simba itaondoka nchini humo ikiwa imecheza mechi nne za kirafiki, ikishinda mbili, sare moja na kupoteza moja.

Kwenye mechi ya kwanza, ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Ismailia, kabla ya kuishindilia Abou Hamad mabao 6-0 na kisha mchezo wa tatu ikacheza dhidi ya Haras El Hadoud ya huko na kuibuka na ushindi wa mabao 2-0, kabla ya kumalizia hasira zao kwa Al Kholood ya Saudi Arabia.

Simba ilikuwa nchi Misri kwa takriban majuma matatu, tangu Julai 14, ikijifua chini ya kocha mpya Zoran ambaye anakiandaa kwa ajili ya Ligi ya Mabingwa, Ligi Kuu, Kombe la FA, na mashindano mengine.

Kuhusu mazungumzo ya kusitisha mikataba kati ya wachezaji Meddie Kagere, Chris Mugalu, na Thadeo Lwanga, alisema yamekamilika na mambo yamekwenda vizuri na huenda kilichoamulia kikatangazwa wakati wowote kuanzia leo.

"Mazungumzo yamekamilika, muafaka umefikiwa, masuala ya kisheria na mikataba yamejadiliwa na kila kitu kimekwenda vizuri kilichobaki ni kutoa taarifa, kila Mwanasimba atafahamu mustakabali wao," alisema Meneja huyo.

## Malele kutangazwa kuinoa JKT Tanzania

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa JKT Tanzania umeweka wazi uko katika hatua za mwisho za mazungumzo na Kocha Hamsini Malele kwa ajili ya kukinoa kikosi cha timu hiyo kuelekea msimu mpya wa Championship 2022/23.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa JKT Tanzania, Abdul Nyumba alisema wakati wowote kuanzia sasa watakuwa wamekamilisha suala la kocha huyo na kuweka wazi muda wa mkataba wake.

Alisema malengo makubwa ya kuimarisha benchi la ufundi ni kuhakikisha msimu huu, wanafanikiwa kuipandisha timu na kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tunatarajia kuwa na Malale ambaye atakuwa kocha wetu mkuu kwa sababu kila kitu kinaenda vizuri na muda wowote tutamtangaza rasmi kukinoa kikosi cha timu yetu," alisema Nyumba.

## Zimamoto kujichimbia wiki mawindo Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Zimamoto inatarajia kuweka kambi ya wiki moja ikiwa ni maandalizi ya kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar ambapo inatarajia kuanza mwishoni mwa mwezi huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mohmed Ali Hilali 'Kocha Tedy', alisema timu hiyo huenda ikaweka kambi hapa hapa visiwani Zanzibar au Tanzania Bara kwa ajili ya maandalizi hayo ya msimu mpya.

Alisema mipango ya timu hii kwa msimu huu ni kuhakikisha inafanya vizuri tofauti na msimu uliyopita ambao ilimaliza nafasi ya tano katika msimamo wa ligi hiyo.

"Tumeanza mazoezi ya kujifua kuelekea msimu mpya wa ligi, najua kwamba ligi itakuwa ngumu ikilinganishwa na msimu uliopita, hivyo tunatakiwa tuwe na jitihada kwa wachezaji kufanya mazoezi kwa mujibu wa mpangilio wa mwalimu," alisema.

Aidha, alisema timu hiyo katika maandalizi yake inatarajia kucheza mechi tano za kirafiki ili kupata muunganiko mzuri kati ya wachezaji wapya ambao wamesajili msimu huu na wale wa zamani.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### WALINZI SITA KUUZWA UNITED

KLABU ya Manchester United inatazamia kuwauza mabeki sita kabla ya dirisha la usajili kukamilika mwezi huu. ***(Mail)***

### BAILLY AMKATAA MOURINHO

MLINZI Manchester United na Ivory Coast, Eric Bailly mwenye umri wa miaka 28, amekataa kuungana tena na Kocha Jose Mourinho katika Klabu ya AS Roma akipendelea kuhamia Sevilla. ***(Sun)***

### BATSHUAYI KUTUA EVERTON

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Ubelgiji, Michy Batshuayi mwenye umri wa miaka 28, yuko tayari kuhamia Everton msimu huu wa majira ya joto. ***(Talksport)***

### MADDISON BEI JUU

KLABU ya Leicester City wameiambia Newcastle United kwamba, watahitaji kulipa pauni milioni 60 kama wanataka kumsajili, James Maddison mwenye umri wa miaka 25. ***(Football Insider)***

### SCHMEICHEL HUYOOO NICE

GOLIKIPA na nahodha wa Leicester, Kasper Schmeichel mwenye umri wa miaka 35, anakaribia kujiunga na Nice ya Ufaransa na atafanyiwa vipimo vya afya wiki hii, na hivyo kuhitimisha miaka 11 ya kukaa England. ***(Mail)***

### WERNER KUTUA LEIPZIG

KLABU ya RB Leipzig inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Chelsea na Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 26 mbele ya Juventus. ***(Mail)***

### GVARDIOL ATAKIWA CHELSEA

KLABU ya Chelsea inamtaka beki wa Leipzig na Croatia, Josko Gvardiol mwenye umri wa miaka 20. ***(Fabrizio Romano)***

### SESKO AVUTIA KIBAO ULAYA

KLABU ya Red Bull Salzburg ipo tayari kutoa ofa zaidi ya pauni milioni 45 kwa fowadi wa Slovenia, Benjamin Sesko mwenye umri wa miaka 19, ambaye analengwa na Manchester United, Chelsea na Newcastle. ***(Sport)***

### SARR AZUIWA CHELSEA

CHELSEA wamezuia mpango wa Fulham kumnunua beki Mfaransa, Malang Sarr mwenye umri wa miaka 23. ***(Standard)***

### ARRIZABALAGA ANUKIA NAPOLI

KLABU ya Napoli ipo kwenye mazungumzo na Chelsea kuhusu kumsajili kwa mkopo kipa wa Hispania, Kepa Arrizabalaga mwenye umri wa miaka 27. ***(Sky Sports)***

### SLONINA ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA wanakaribia kukamilisha usajili wa mlinda mlango wa Marekani, Gabriel Slonina mwenye umri wa miaka 18 kutoka Chicago Fire, ambapo atasalia kwa mkopo hadi Januari. ***(Fabrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO: LUKAKU NA MARTINEZ PATINA BORA

**Wanaweza kuwa na upatina mzuri zaidi, hisia nyingi, malengo mengi, lakini Dybala naye...**

**MILAN,** Italia

RONALDO de Lima amepongeza kitendo cha Inter Milan kumsajili Romelu Lukaku na anaamini kuwa ushirikiano na Lautaro Martinez utakuwa "bora zaidi."

**Lukaku ambaye ni mshambuliaji wa kimataifa wa Ubelgiji amerejea Inter Milan baada ya msimu wa kukatisha tamaa akiwa na Chelsea, ambapo hakuwapo kwenye kikosi cha kwanza cha kocha, Thomas Tuchel na alikiri hadharani kuwa anataka kurudi Nerazzurri.**

Hatua hiyo ilitimia katika dirisha la sasa, huku Lukaku akiwasili kwa mkopo, akiwa amefunga mabao 30 katika michuano yote wakati wa kampeni ya Inter ya kushinda taji la Serie A msimu wa 2020-21.

Ronaldo anaamini Inter wangetetea taji lao kama Lukaku angesalia katika klabu hiyo msimu uliopita, wakati Milan ilipolitwaa.

"Utakuwa ushirikiano mzuri kati ya Lukaku na Martinez," alisema Ronaldo nyota wa zamani wa Brazil akiliambia Gazzetta dello Sport.

"Lukaku na Lautaro wanaweza kuwa na upatina mzuri zaidi. Hisia nyingi, malengo mengi."

Ronaldo, ambaye aliichezea Inter kutoka mwaka 1997 hadi 2002, pia alielezea mawazo yake juu ya hali hiyo na Paulo Dybala, ambaye alikuwa akihusishwa sana na Nerazzurri baada ya kumalizika kwa mkataba wake na Juventus, lakini akajiunga na Roma.

"Katika soka huwezi kila wakati kufanya kile unachotaka na labda unataka kitu fulani, lakini unajiwekea mipaka. Dybala nae angekuwa muhimu kwa Inter kama angejiunga nao," alisema.

Kuimarika kwa safu ya ushambuliaji kwa Inter kunatazamiwa kuendelea baada ya kuondoka kwa Alexis Sanchez, ambaye inasemekana kuwa amekubali kujiunga na Cesc Fabregas katika Klabu ya Serie B ya Como.

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,019,3

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 03 AGOSTI 2022
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 03/08/22 | 20:00 | Landskrona Bois vs Skovde Aik | 2.28 | 3.47 | 3.01 |
| 02. 03/08/22 | 20:00 | Dalkurd FF vs Norrby IF | 2.96 | 3.57 | 2.26 |
| 03. 03/08/22 | 21:30 | Dunajska Streda vs Steaua Bucuresti | 2.62 | 3.33 | 2.57 |
| 04. 04/08/22 | 03:00 | Juarez FC vs San Luis | 2.52 | 2.92 | 2.97 |
| 05. 04/08/22 | 18:30 | AEK Larnaca vs Partizan | 3.17 | 3.22 | 2.25 |
| 06. 04/08/22 | 19:00 | Stjordals-Blink vs Grorud IL | 2.60 | 3.43 | 2.36 |
| 07. 04/08/22 | 19:00 | Sandnes Ulf vs Sogndal | 2.33 | 3.48 | 2.60 |
| 08. 04/08/22 | 19:30 | Spartak Trnava vs Rakow Czestochowa | 3.02 | 3.33 | 2.28 |
| 09. 04/08/22 | 20:00 | Jonkopings Sodra vs Vasteras SK | 2.40 | 3.57 | 2.76 |
| 10. 04/08/22 | 20:30 | Zorya Lugansk vs Universitatea Craiova | 2.62 | 3.18 | 2.67 |
| 11. 04/08/22 | 21:00 | Sepsi Osk vs Djurgardens IF | 2.58 | 3.24 | 2.68 |
| 12. 04/08/22 | 21:30 | Brondby vs FC Basel | 2.56 | 3.37 | 2.61 |
| 13. 04/08/22 | 22:00 | Hajduk Split vs Vitoria Guimaraes | 2.57 | 3.33 | 2.62 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa
airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# FABREGAS ASAJILIWA ITALIA

**ROME,** Italia

KIUNGO wa zamani wa Hispania, Cesc Fabregas, amejiunga na Klabu ya Serie B ya Como kwa uhamisho wa bure kutoka Monaco.

Nyota huyo wa zamani wa Arsenal, Barcelona na Chelsea, aliripotiwa kufikiria kustaafu baada ya kuondoka kwenye kikosi cha Ligue 1 mwezi uliopita, lakini amechagua kuendelea na soka lake kwa kusaini mkataba wa miaka miwili na Como.

Akizungumza wakati wa utambulisho wake, Fabregas alifichua kwamba alishawishiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa klabu na mchezaji wa zamani wa Chelsea, Dennis Wise.

"Nilikuja hapa kucheza kwa njia bora zaidi na kushinda michezo mingi iwezekanavyo. Hiki ndicho kipaumbele changu na kama ningehisi kwamba sivyo tena, ningetundika buti zangu," alisema Fabregas.

"Nataka kuipeleka Como pale inapostahili kuwapo, kwenye Serie A. Niliamua kuja hapa kwa sababu nyingi.

"Nilitaka mradi ambao ungenipa shauku, sikufuata fedha. Wise ndiye aliyenishawishi zaidi na mimi nikahamasika.

"Nadhani hii ni moja ya changamoto muhimu zaidi katika maisha yangu ya soka."

Fabregas aliongeza kuwa kuhamia Como pia ulikuwa "mradi bora zaidi kuliko kwenda Ligi Kuu ya Marekani, MLS.



# Ramsey atua Nice bure

**NICE,** Ufaransa

AARON Ramsey amejiunga na timu ya Ligi Kuu ya Ufaransa, Nice kwa uhamisho huru baada ya mkataba wake na Juventus kuvunjwa.

Juve walithibitisha kutengana na nyota huyo wa Wales wiki iliyopita baada ya kuandamwa na majeraha nchini Italia, lakini kuhamia kwake Ufaransa kunampa nafasi ya kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara kabla ya michuano ya Kombe la Dunia.

Ramsey alicheza mechi 70 katika mashindano yote akiwa na 'Bianconeri', akifunga mabao sita, lakini ni mechi tano tu kati ya hizo alizocheza msimu wa 2021/22.

Majeraha yalitatiza muda wake chini ya kocha Massimiliano Allegri na kisha akapelekwa kwa mkopo Rangers, ambako alishinda Kombe la Scotland na kucheza fainali ya Ligi ya Europa.

Anajiunga na timu ya Nice inayotaka kuimarika hadi kumaliza katika nafasi ya tano kwenye Ligue 1 msimu uliopita na kufuzu kwa raundi ya mchujo ya Ligi ya Europa.

301,493/-

# MANDONGA: MTU KAZI MAARUFU KWA VIPIGO

• Sasa kuanza kununuka hela ndefu

Na Adam Fungamwango

"SHAABAN Kaoneka, kazi unayo, hapa umeyakanyaga, umekutana na Mandonga Mtu Kazi, utajuta kuzaliwa, aliyekushawishi, utajilaumu, utapigwa ndonga utalala, hapa chinja ua."

**"Shaaban kadandia mtumbwi wa kibwengo. Mtumbwi wa kibwengo ni mtumbwi wa vibwengo tu, huwa hauvushi binadamu mtoni, ukidandia utakufa tu."**

Hizo ni tambo na vitisho vya bondia aliyejizolea umaarufu kwa muda mfupi tu, Karim Mandonga kutoka mkoani Morogoro. Kwa sasa ndiyo habari ya mjini. Mitandao ya kijamii, mitaani pamoja na kuzungumzia usajili wa klabu za Simba na Yanga, udhamini, lakini Mandonga ndiye amekuwa akizungumziwa, zaidi akijizolea mashabiki wengi kwa namna ambayo imewashangaza watu wengi. Na hata hao wanaoshangaa na kupata habari zake, wanajikuta wakiangua vicheko nao pia wanajiunga na mashabiki wake.

Hapo alikuwa akimpiga mkwara bondia Shaaban Kaoneka kabla ya pambano lao lililofanyika Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Majimaji, Songea mkoani Ruvuma.

Lilikuwa ni pambano la raundi sita na uzito wa Super Middle Weight, ambalo ndilo lilikuwa maarufu zaidi kuliko pambano 'mama' la WBF Super Middle la kilo 76 kati ya Selemani Kidunda na Erick Katompa kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

### MIKWARA YAKE

"Wanangu wa Songea na Morogoro, nataka niwape zawadi, nawapigia KO, raundi ya kwanza, 'kata goli', Mandonga Mtu Kazi, karudi kazini.

Nasikia eti jamaa kaja na sumu anataka kunipa mimi Mandonga, dawa ya sumu ni maziwa, ninayo mimi, nasema hivi, tutachukua jeneza tutamweka, halafu tutakwenda kuzika yeye, tunampiga KO na lazima liandaliwe jeneza."

Ni sauti nzito ya msisitizo ya kile anachokisema, ikitoka kwa Mandonga kabla ya pambano hilo.

Ndiye bondia pekee aliyepewa gari aina ya Jeep kuzunguka Songea yote kutangaza pambano lake na kujinadi.

Umaarufu wa Mandonga ulianza kuchipuka Machi mwaka huu, alipompiga mkwara mkali bondia Magambo Christopha, lakini kwenye pambano lenyewe alipigwa raundi ya kwanza tu.

Kabla ya pambano la Jumamosi, alianza kuteka vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, kutokana na matangazo yake, video fupi zikitoka zikimwonyesha akibeba magogo, kukimbia mchangani na kupiga ngumi miti hadi magamba yananyofoka.

Akajizolea rundo la mashabiki kila anapopita toka Morogoro hadi alipotua Songea, kila mtu akitaka kumwona na kupiga naye picha.

### ALIVYOKONG'OTWA

Kama kawaida yake, aliingia kwa mbwebwe, huku mashabiki wake wakiwa na mabango mbalimbali, lakini moja kubwa liliandikwa 'Mandonga Bendera ya Kuzimu'.

Aliweza kuhimili raundi mbili za mwanzo. Ilipofika ya tatu hali ilianza kubadilika alianza kusukumiwa makonde, lakini alihimili. Mashabiki wake waliendelea kumshangilia kama kawaida yao hata wakati anasukumiwa makonde wao waliimba 'Mandonga, Mandonga.'

Miguu ilianza kusaliti kwenye raundi ya tatu kwani ilionekana kuanza kutetemeka na akitembea huku akiyumba akielekea kukaa kwenye kigoda, baada ya raundi hiyo kumalizika.

Dakika ya kwanza na sekunde 30 ya raundi ya nne, alipigwa ngumi kali na kuanguka chini kama gunia. Aliinuka na kuendelea, lakini miguu iliendelea kuwa kikwazo. Sura yake ilikuwa inajieleza, haikuwa na nuru tena, aliaza kukata tamaa.

Kaoneka na aligundua hilo, akaanza kumvurumishia makonde bila yeye kujibu, mikono ikiwa chini, kitu ambacho ni cha hatari kwenye ngumi, mwamuzi akasimamisha pambano kumwokoa Mandonga. Akapigwa TKO raundi ya nne.



### AENDELEZA SHOMBO

"Kaoneka ni bondia mdogo sana, siyo wa kumpiga Mandonga ndiyo ajione mkubwa, ni bondia mdogo na muoga. Nataka mechi ya marudiano naye na si yeye, wote walionipiga, nawataka. Septemba nimeandaliwa pambano na Mkongomani." Yalikuwa ni maneno yake baada ya pambano kumalizika.

"Nimeumia kiasi kikubwa sana, kwa sababu kuna watu wameniandaa, wamefunga safari zao kumuona Mandonga mtu kazi, lakini hajawaonyesha, amewanyong'onyeza kwa kiasi fulani, naomba sana samahani sana kwa watu wangu, michezo ndiyo ilivyo, michezo haina ahadi, nitaendelea kupambana kwenye mazoezi na haya yaliotokea leo mimi nitawalipa, waniwekee matumaini yao, nitawalipa kwa hilo na ngumi sitaacha," alisema.

Pamoja na kupigwa, mashabiki wote wa Mandonga wameonekana kuendelea kumuunga mkono na kuendelea kujizolea idadi kubwa nyingine ya mashabiki baada ya mechi hiyo.

"Tuko pamoja na Mandonga, tutamuunga mkono kwenye mapambano yake yote, hata akipigwa mpaka kufa," ni kaulimbiu ya mashabiki wake.

### UMAARUFU WAMLIPA

Kwa sasa Mandonga ndiye bondia maarufu zaidi nchini.

"Nashangaa huko nyuma nimewapiga mabondia wengi, lakini baada ya kupigwa nimepata jina sana, hadi nimepewa mchuma huu mwanangu," alisema bondia huyo.

Tayari baadhi ya kampuni na taasisi zimeanza kumtumia kwenye matangazo yao na yamekuwa yakivutia wengi.

Afande Sele, msanii wa Morogoro amesema Mandonga ni tunu kwa sasa, kwani ameuchangamsha mchezo wa ngumi na kwa sasa mapambano hayawezi kuwa mazuri bila yeye kuwamo, amekuwa ni bidhaa adimu.

"Ni rafiki yetu sisi Morogoro tunamjua anaweza kuwa balozi mzuri wa ndondi nchini, ana dhamira, atafute mwamuzi mzuri na akae na mabondia wengine ili kupata ushirikiano na maarifa, bado umri unamruhusu, hata George Foreman alitwaa ubingwa wa dunia akiwa na umri mkubwa," alisema.

## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 06/08/22 | 17:00 | Leeds vs Wolverhampton | 2.29 | 3.29 | 3.09 |
| 02. 06/08/22 | 17:00 | Bristol City vs Sunderland | 2.21 | 3.24 | 3.29 |
| 03. 06/08/22 | 17:00 | QPR vs Middlesbrough | 2.47 | 3.24 | 2.84 |
| 04. 06/08/22 | 17:00 | Reading vs Cardiff | 2.44 | 3.18 | 2.94 |
| 05. 06/08/22 | 17:00 | Swansea vs Blackburn | 2.36 | 3.19 | 3.04 |
| 06. 06/08/22 | 17:00 | Burton vs Bristol Rovers | 2.39 | 3.33 | 2.88 |
| 07. 06/08/22 | 17:00 | Charlton vs Derby | 2.79 | 3.19 | 2.54 |
| 08. 06/08/22 | 17:00 | Exeter vs Port Vale | 2.53 | 3.17 | 2.82 |
| 09. 06/08/22 | 17:00 | Fleetwood Town vs Plymouth | 2.84 | 3.24 | 2.48 |
| 10. 06/08/22 | 17:00 | MK Dons vs Sheffield Wed | 2.61 | 3.21 | 2.71 |
| 11. 06/08/22 | 17:00 | Shrewsbury vs Accrington | 2.53 | 3.23 | 2.78 |
| 12. 06/08/22 | 17:00 | Barrow vs Bradford City | 2.59 | 3.13 | 2.78 |
| 13. 06/08/22 | 17:00 | Crawley Town vs Leyton Orient | 2.58 | 3.22 | 2.73 |
| 14. 06/08/22 | 17:00 | Hartlepool vs AFC Wimbledon | 2.89 | 3.24 | 2.44 |
| 15. 06/08/22 | 17:00 | Mansfield vs Tranmere | 2.26 | 3.19 | 3.24 |
| 16. 06/08/22 | 18:00 | Strasbourg vs Monaco | 2.73 | 3.23 | 2.53 |
| 17. 06/08/22 | 21:30 | Hansa vs Arminia Bielefeld | 2.64 | 3.34 | 2.59 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 03 - AGOSTI 2022

| MUDAVV | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:30 | 1110 | Sydney Utd vs Monaro Panthers | 1.44 | 4.61 | 5.29 |
| 12:30 | 3133 | Western United vs Melbourne Victory | 2.96 | 3.40 | 2.14 |
| 12:30 | 3896 | Devonport Strikers vs Wellington Phoenix | 7.63 | 5.87 | 1.25 |
| 12:30 | 4945 | Brisbane Roar Youth vs Capalaba FC | 1.42 | 5.08 | 5.08 |
| 13:00 | 4473 | Sanfrecce Hiroshima vs Yokohama F Marinos | 2.38 | 3.38 | 2.60 |
| 13:00 | 4846 | Incheon Utd vs Suwon City | 2.70 | 3.19 | 2.40 |
| 13:00 | 5097 | Cerezo Osaka vs Kawasaki Frontale | 2.81 | 3.25 | 2.29 |
| 13:00 | 5732 | Vissel Kobe vs Avispa Fukuoka | 1.99 | 3.14 | 3.58 |
| 13:30 | 1360 | Gangwon vs Jeonbuk Hyundai | 3.10 | 3.29 | 2.11 |
| 13:30 | 3163 | Daegu vs Suwon Samsung | 2.14 | 3.04 | 3.29 |
| 13:30 | 3297 | Nagoya Grampus vs Urawa Red Diamonds | 2.70 | 3.04 | 2.50 |
| 14:30 | 2031 | Jinan Xingzhou vs Zibo Qisheng | 1.28 | 4.92 | 8.66 |
| 14:45 | 5628 | Geylang Int. vs Tampines | 3.00 | 3.80 | 2.06 |
| 17:00 | 3338 | Otmk Olmaliq vs Metallurg Bekabad | 1.64 | 3.19 | 5.69 |
| 17:35 | 1936 | Lekhwiya SC vs AL Wakrah | 1.65 | 4.11 | 4.02 |
| 18:00 | 2485 | Lokomotiv Tashkent vs Qizilqum | 2.06 | 3.05 | 3.49 |
| 19:00 | 2258 | Kristiansund vs Tromso | 2.86 | 3.46 | 2.30 |
| 19:00 | 4425 | VSK Arhus vs Vendsyssel FF | 7.86 | 5.11 | 1.29 |
| 19:00 | 4891 | Bodo Glimt vs Zalgiris | 1.32 | 5.01 | 8.02 |
| 19:00 | 5664 | Karabakh vs Ferencvaros TC | 2.07 | 3.30 | 3.40 |
| 19:30 | 4682 | Regensburg II vs TSV Grossbardorf | 1.63 | 4.12 | 4.12 |
| 19:45 | 4725 | Al Rayyan SC vs Al-Shamal | 1.56 | 4.12 | 4.61 |
| 20:00 | 1364 | Landskrona Bois vs Skovde Aik | 2.52 | 3.41 | 2.70 |
| 20:00 | 1513 | VfB Lubeck II vs TSV Pansdorf | 2.70 | 4.10 | 2.15 |
| 20:00 | 1907 | Trelleborgs FF vs Halmstads BK | 3.36 | 3.41 | 2.13 |
| 20:00 | 2967 | Brommapojkarna vs Orebro SK | 1.78 | 3.87 | 4.17 |
| 20:00 | 4064 | Maccabi Haifa vs Apollon Limassol | 1.58 | 3.84 | 5.39 |
| 20:00 | 4128 | FC Riga vs Gil Vicente | 3.68 | 3.53 | 1.94 |
| 20:00 | 4382 | Dalkurd FF vs Norrby IF | 3.12 | 3.52 | 2.20 |
| 20:00 | 4778 | Viborg FF vs B36 Torshavn | 1.17 | 6.66 | 15.14 |
| 20:00 | 5173 | IK Brage vs Ostersunds | 1.60 | 4.07 | 5.29 |
| 20:30 | 3602 | Wolfsberger AC vs Gzira United | 1.21 | 6.04 | 13.08 |
| 21:00 | 1006 | EC XV De Jau U20 vs Corinthians SP U20 | 4.72 | 3.59 | 1.64 |
| 21:00 | 1391 | Arna-Bjornar W vs Sandviken W | 39.36 | 12.79 | 1.01 |
| 21:00 | 1549 | Chalatenango vs CD Aguila | 2.85 | 2.80 | 2.55 |
| 21:00 | 2618 | Santa Tecla vs Firpo | 2.34 | 3.00 | 2.95 |
| 21:00 | 2731 | EC Agua Santa SP U20 vs Guarani SP U20 | 2.70 | 3.15 | 2.55 |
| 21:00 | 2891 | Isidro Metapan vs Jocoro FC | 1.99 | 3.00 | 3.78 |
| 21:00 | 3138 | Dynamo Kiev vs Sturm Graz | 2.12 | 3.29 | 3.29 |
| 21:00 | 3229 | Noroeste SP U20 vs Mirassol FC U20 | 3.50 | 3.25 | 2.05 |
| 21:00 | 5510 | Penapolense SP U20 vs Palmeiras SP U20 | 5.48 | 4.40 | 1.45 |
| 21:00 | 5579 | SAO Caetano SP U20 vs Desportivo Brasil U20 | 3.43 | 3.43 | 1.93 |
| 21:00 | 5772 | FC Aguablanca vs Deportes Quindio | 4.68 | 3.01 | 1.81 |
| 21:00 | 5932 | CD Atletico Marte vs CD FAS | 2.91 | 3.05 | 2.33 |
| 21:30 | 1812 | Dunajska Streda vs Steaua Bucuresti | 2.88 | 3.34 | 2.36 |
| 21:45 | 4631 | Red Star Belgrade vs Pyunik Yerevan | 1.16 | 6.40 | 16.01 |
| 22:00 | 2342 | Al Ahly Cairo vs Farco FC | 1.31 | 4.82 | 9.84 |
| 22:15 | 2739 | Vikingur Reykjavik vs Leiknir | 1.28 | 5.30 | 7.85 |
| 22:15 | 4205 | Fram Reykjavik vs Stjarnan | 2.80 | 3.59 | 2.15 |
| 22:15 | 5489 | Valur vs Hafnarfjordur | 2.02 | 3.54 | 3.09 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatano Agosti 3, 2022
Nipashe



Mandonga: Mtu Kazi maarufu kwa vipigo UKURASA 23

MSAADA...




Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Simba, Barbara Gonzalez, akimkabidhi sabuni mmoja wa wazee wanaoishi katika Kituo cha Wazee Nunge kilichoko Kata ya Vijiweni Jimbo la Kigamboni, Dar es Salaam, Mohamed Ally, mwenye miaka 82, baada ya viongozi, wanachama na mashabiki wa timu hiyo kutembelea kituoni hapo jana kwa ajili ya kutoa misaada ikiwa ni utaratibu wao wa kila mwaka kuelekea Tamasha la Simba Day Agosti 8. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Yanga kumtesti Aziz Ki kwa KMC FC leo

**Khadija Mngwai na Shufaa Lyimo**

## Usajili mpya wote ndani, kilele cha Mwananchi chapamba moto, wagawa misaada...

WAKATI uongozi wa Klabu ya Yanga na wanachama wakiendelea na maandalizi ya kuelekea kilele cha Siku ya Mwananchi ambayo inaenda sambamba na kugawa misaada mbalimbali kwa jamii, nyota wapya wa kikosi hicho akiwamo, mshambuliaji mpya, Stephane Aziz Ki, leo watapata nafasi ya kuonja joto mojawapo la wapinzani wao wa Ligi Kuu Bara watakapoivaa KMC FC katika mchezo wa kirafiki.

**Yanga inatarajia kusherehekea Siku ya Mwananchi Jumamosi wiki katika Uwanja wa Benjamin Mkapa ambapo pia itacheza mechi ya kirafiki dhidi Mabingwa wa Ligi Kuu Uganda, Vipers SC ikiutumia mchezo huo kutambulisha wachezaji wake wa msimu ujao.**

Hata hivyo, katika maandalizi ya mchezo huo, leo itaikaribisha KMC FC kwenye mechi ya kirafiki itakayopigwa kambini kwa Yanga, Avic Town iliyoko Kigamboni, Dar es Salaam.

Yanga ambayo inaendelea na maandalizi ya msimu mpya wa 2022/23 unaotarajiwa kuanza Agosti 17, mwaka huu, pia itafungua msimu mpya wa ligi hiyo kwa kucheza dhidi ya watani wao, Simba kwenye mechi ya Ngao ya Jamii ikitakayochezwa Agosti 13 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Akizungumza na Nipashe jana, Daktari wa Yanga, Shecky Mngazija alisema kikosi chao kinatarajia kujipima na KMC katika Uwanja wa Avic Town leo wakijiandaa na kilele cha Siku ya Mwananchi na kwamba Kocha Nasreddine Nabi atautumia mchezo huo kuendelea kuwapima wachezaji wake wapya.

"Leo (jana) kikosi kimefanya mazoezi ya gym kwa ajili ya wachezaji kujiweka fiti, ikiwa ni maandalizi ya mechi ya kirafiki dhidi ya KMC, mchezo tunaotarajia kuchezwa katika uwanja wa kambi yetu ya Avic Town saa 10.30 jioni.

"Maandalizi yanakwenda vema na lengo la kucheza mechi za kirafiki ni kuhakikisha tunafanya vizuri katika mchezo wetu wa Wiki ya Mwananchi dhidi ya Vipers," alisema.

Katika hatua nyingine, Rais wa Klabu ya Yanga, Hersi Said, jana amekabidhi vifaa mbalimbali vya shule katika Sekondari ya Jangwani pamoja na taulo za kike ikiwa ni mwendelezo wa kuisaidia jamii kuelekea kilele cha Siku ya Mwananchi.

Akizungumza wakati akikabidhi vifaa hivyo, Hersi alisema ametoa vifaa hivyo kutokana na kutambua umuhimu wa elimu.

"Huu ni mwendelezo wa wiki yetu ya Mwananchi ndio maana tumeamua kutoa vifaa hivi kwa wanafunzi pamoja na vifaa vya walimu," alisema.

Alisema leo kutakuwa na mbio za CRDB ambazo zitakuwa mahususi kwa wanawake wajawazito pamoja na watoto wenye matatizo ya moyo.

Mbali na hayo Alhamisi watakuwa na zoezi la kuchangia damu wakishirikiana na mdhamini wao mkuu SportPesa, ambalo litafanyika makao makuu ili kuisaidia Hospitali ya Taifa Muhimbili huku Ijumaa ikiwa ni dua kabla ya Jumamosi kuhitimisha kilele hicho Uwanja wa Mkapa.

# Simba yaanza vitisho Yanga

**Na Saada Akida**

HUKU Simba ikiendelea na matukio ya Simba Day, uongozi wa klabu hiyo umeweka wazi kwamba kuna jambo kubwa zaidi ndani ya Agosti hii ikiwamo mikakati ya kutwaa taji la Ngao ya Jamii, dhidi ya Yanga.

Simba wako nchini Misri kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa mashindano ikiwa ni pamoja na mchezo huo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Yanga utakaopigwa Agosti 13, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Kauli hiyo imetolewa na viongozi wa Simba baada ya kutembela kituo cha wazee Nunge kilichoko Kata ya Vijiweni, Kigamboni jijini Dar es Salaam jana na kutoa msaada wa unga wa ngano, mchele, mafuta na sabuni.

Kituo hicho ambacho kilianzishwa mwaka 1936 na mkoloni kwa ajili ya kuwatunza waathirika wa ugonjwa wa ukoma, kina wazee 22, huku 12 wakiwa wanaume na wanawake 10.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Simba, Ahmed Ally, alisema kwamba msimu huu wamejipanga vizuri kuhakikisha Simba hawapotezi kama ilivyo kwa msimu uliopita.

"Tumekuja kuleta msaada kwa wazee kwa ajili ya kupata baraka zenu, kwa sababu msimu huu tumejipanga vizuri, baada ya udhamini mkubwa tuliotangaza juzi, kuna moto unaokuja, Siku ya Simba Day na balaa zaidi siku ya Ngao ya Jamii," alisema Ahmed Ally.

Naye Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema Simba inaonyesha ukaribu wake kwa jamii na wameamua kuja kwenye kundi hili lililosahaulika kwa sababu wanajua thamani yao.

"Tumesikia changamoto zilizoko ikiwamo uzio na paa, tumemwomba ofisa ustawi atuletee taarifa tuone tutawasaidiaje, tuna malengo mengi kuanzia Agosti 8 na 13 pamoja na msimu mzima.

"Mwisho wa mwezi huu ratiba ya Ligi ya Mabingwa inaenda kutoka tunaenda kuanzia raundi ya pili naamini tunaenda kushinda na kutinga makundi," alisema Barbara.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >